# *Siye Mimi Niliyekutuma?*

Asante, ndugu yangu. Bwana akubariki.

2 Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa, usiku wa leo, katika kanisa hili zuri, dogo, linaloonekana kistarehe. Na—na kwa hiyo nina hakika Roho Mtakatifu yuko hapa, na Yeye ana—Yeye anaufahamu umati huu wote, kwa hiyo tuna furaha tu kuwa hapa kuketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukifurahia ushirika huu mzuri sana.

3 Kwa hiyo sisi, tunataka kutangaza ya kwamba kesho usiku sasa ni, m—mkutano utaanza kesho usiku, huko Ramada. Nadhani jumba la mikutano liko papo hapo pamoja na... Naam, bwana. Na kila mtu anayeweza, ajitokeze kwa kila ibada. Nadhani Ndugu Williams amelipitia, katika utaratibu, na kusimulia yote yaliyotukia, yote yaliyotukia, na yatakayotukia, kadiri ajuavyo yatakayotukia. Maana wakati mwingine katika mikutano hii, jambo fulani hutukia ambalo hatuninii, kamwe hatujui, tunaenda kule tukitazamia jambo fulani kutukia. Na mara ya mwisho hakika tulikuwa na ushirika mzuri sana kule Westward Ho, ninaamini ndivyo kuliitwa, Westward Ho.

4 Na sasa, kwa kuwa nadhani imetangazwa, ya kwamba kesho usiku Ndugu yetu mpendwa Oral Roberts atakuwa akizungumza, kesho usiku, Bwana akipenda. Na kutakuwako na wengi zaidi kule, nanyi mtawasikia wahubiri mashuhuri, baadhi ya wafanyabiashara, wahudumu kutoka kila mahali. Sijui hata mmoja wa wahubiri waliotangazwa nje ya Ndugu Gardner, pia ninamjua Ndugu Velmer Gardner. Na kwa hiyo, wako na kuanzia sasa hadi Jumatatu usiku, kwa hiyo tunatarajia tu yubile kubwa mno ya ulaji wa kiroho, kwa hiyo—kwa hiyo sisi, tunakuja na kula mambo ya Bwana.

5 Na sasa, nafikiri kura inaniangukia kwa ajili ya Jumapili, ama, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Jumamosi asubuhi, na kwa ajili ya ibada ya Jumapili alasiri, na kadhalika, kuzungumza.

6 Sasa, ninataka kusema ya kwamba huu umekuwa mmoja wa nyakati nzuri sana nilizowahi kuwa nazo huku Phoenix. Kwa kawaida, ninapokuwa Phoenix mimi huenda tu, labda, ninaenda mahali pamoja, lakini wakati huu, nafikiri hizi ni kama sehemu sita ama saba, labda nane ambazo nimepitia, kote kupitia Mto Salt, tisa, sehemu tisa ambazo nimekuwa, sehemu tisa mbalimbali, hao ni wahudumu tisa mbalimbali wa kufahamiana nao, kuwapa mikono, na kufanya ushirika na madhehebu mbalimbali.

7 Mbona, kwa kawaida ninapoingia, mbona, hao ndugu, daima ni wazuri sana, nao wanayaachilia makanisa yao na kuingia. Nafikiri ni vizuri kwa—kwa, hasa, wainjilisti wanaoingia, na—

na kutumia wakati wao kujaribu kusaidia kila kanisa, kisha kuzunguka na kuyatembelea makanisa namna hiyo, maana mchungaji daima yuko tayari kushirikiana, nao watu wao wanakuja na kupata, labda, kuombewa, ama jambo fulani likatendeka, ama mtu fulani anaokolewa, halafu basi anamjua mtu huyo, wahudumu mbalimbali wanasema, "Vema, huyu Ndugu *Nanii*, kama uko katika wilaya hiyo, mbona, mwendee moja kwa moja, mtu mzuri sana wa Mungu, nimekuwa kanisani mwake."

8 Nanyi mwajua, na—napenda hilo, nafikiri tunapata kufahamiana zaidi mmoja na mwenzake, na kwa sababu tutakuwa na Umilele wa kuishi pamoja, kwa hiyo afadhali tufahamiane huku chini na kujua jinsi kulivyo.

9 Na kwa hiyo—kwa hiyo basi, huko juu, jambo moja zuri hata hivyo, Ndugu Mchungaji, kwa namna fulani hatutakuwa tu, hatutakuwa na mkutano wowote wa maombi, la, hatutakuwa na ibada zozote za uponyaji, lakini sisi . . . wala hatutakuwa na kikomo cha wakati, kwa hiyo, nami kwa kawaida huhubiri saa sita au nane tu kwa wakati mmoja, labda wakati mwingine, kwa hiyo basi ninaweza tu kuendelea, mwajua.

10 Loo, ninataka kuzungumza na wale niliowahubiria basi! Nilizoea kuwaambia watu kwamba ningependa kuwa na angalau milenia moja na kila mmoja. Mnaona? Halafu basi, nikimaliza . . . Na moja kwa moja katika ibada zetu, zile tu nijuazo, kumekuwa na karibu waongofu milioni mbili ama zaidi wa Kristo, na hapana shaka, wachache wa hao watafaulu kwa vyovyote vile. Na kwa hiyo, kuketi tu chini, labda, tuseme kungekuwako na mia moja wa hao, angalieni jinsi milenia mia moja zingekuwa, kufahamiana tu na watu niliowaongoza kwa Bwana. Ndipo basi mnajua, nitakapomaliza, si—sitakuwa na wakati mmoja pungufu, kuliko wakati nilipoanza. Mnaona?

11 Umilele kamwe hauanzi, hauishi, mnaona, haukuwa na mwanzo, hauna mwisho, huwezi kuuelezea. Lakini chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Kwa hiyo mnasema, "Na sisi je, Ndugu Branham?" Vema, mradi tu wewe ni mwanadamu wa kawaida wa duniani hapa, ulikuwa na mwanzo, lakini kama umezaliwa kutoka Mbinguni, wewe ni sehemu ya Mungu, basi roho hiyo kamwe haikuwa na mwanzo, kwa sababu ni sehemu ya Mungu, ni ya Milele. Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuishi milele, ni kuwa na Uzima wa Milele, hiyo ni kweli, Uzima wa Milele.

12 Lakini kilicho na mwanzo kina mwisho, kwa hiyo kama hukuwa na mwanzo, ninii pekee . . . Mnaona, hapo Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili kwa Roho, hawezi kuingia katika Ufalme, kamwe hawezi kuingia," maana huna budi kuwa na huo Uzima wa Milele.

13 Sasa, bila shaka sininii, sijui vizuri kuzungumza Kiingereza na kujua, nimechunguza neno moja ama mawili ninapoyapata,

nione yalikuwa nini katika Biblia, Kiebrania na Kiyunani, bali neno la Kiyunani hapo la Uzima wa Milele ni neno lile lile lililotumiwa kwa ajili ya Uzima wa Mungu, linaendelezwa Z-o-e, *Zoe*. Naye aliye na Uzima wa Milele ni Zoe, Uzima wa Mungu Mwenyewe. Hilo linakufanya mwana ama binti Yake Mwenyewe, unaona, maana umezaliwa Naye, Uhai Wake uko ndani yako, nawe huwezi kuangamia kama Mungu asivyoweza kuangamia. Kwa hiyo una Uzima wa Milele na, "Nitamfufua katika siku ya mwisho," Mungu alisema. Hilo si ni zuri sana? Hmm! Hmm!

14 Nilikuwa nikiwazia, wakati Mungu, hapo mwanzo, Yeye alinena akasema, "Na iwe," tena, "Na iwe," ikaleta mbegu, kila kitu kwa jinsi yake, unaweza kuchanganya mbegu, bila shaka, na kuigeuza, kama nilivyohubiri hapa Phoenix wakati mmoja juu ya, ninaamini, *Dini Chotara*, jinsi wanavyojaribu kuizalisha na madhehebu, badala ya kuiacha iwe jinsi ilivyokuwa, bali unaacha—unaacha cho—chotara, chochote kilicho chotara hakiwezi kujizaa tena.

15 Kwa hiyo wakati mwanadamu anapokwambia, na ninyi watoto mnaoenda shule, nao wanasema ya kwamba tulitoka kwenye seli moja, na maadili ya Darwin, ka—kamwe hajui analozungumzia, mnaona, kwa sababu ukimchukua farasi na—na ninii, ukichukua, vema, nasema punda na farasi jike, nao wamzae mwa—mwana-punda. Ni—ni nyumbu, bali nyumbu huyo hawezi kumzaa nyumbu mwingine na awe na nyumbu, ameishia papo hapo.

16 Mahindi chotara, ungeweza kuchanganyisha mahindi, halafu ungeweza kupanda mahindi hayo, hayatakuwa chochote, mnaona, hayatakuwa chochote, hayana budi kurudi.

17 Kwa hiyo vipi basi, kama tukianza mageuzi kutoka kwenye seli moja, basi tuko wapi? Mnaona? Utafiti wao wenyewe wa kisayansi unathibitisha kwamba wamekosea. Mnaona? Mnaona, huwezi kufanya hivyo. Unaweza kuzalisha la zambarau ya samawati kwa la zambarau jeupe, upate zambarau ya Kiafrika, bali hebu yaachilie tu, nayo yatarudi moja kwa moja kwenye zambarau ya samawati asili. Hiyo ni kweli. Mnaona? Hayatafanya hivyo.

18 Kwa hiyo wakati Mungu aliponena na kumfanya mwanadamu, na nafsi ya mwanadamu ikapotea, kabisa... Chochote nje ya hayo, kujiunga na kanisa na chochote kile ni kuchanganya mbegu, huna budi kurudi tena, Mungu hana budi kunena Neno tena, hilo linalifanya Uzima wa Milele. Mungu anaponena Uzima ndani yako, basi huo ni wa Milele tena, bali mpaka hapo, ni uchotara, mnaona. Kwa hiyo ibilisi alijichanganyisha nayo na kuichanganya, akajaribu kuchanganya imani na kitu fulani, kutokuamini pamoja, kwa hiyo inafanya chotara, mnaona, na, lakini Mungu anaponena na

kumweka Roho Mtakatifu mle ndani na kulitia muhuri, ni la Milele.

19 Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu," si kanisa takatifu la Mungu, Roho Mtakatifu wa Mungu, "ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Na muhuri unawakilisha kazi iliyomalizika.

20 Hakuna kitu kinachotiwa muhuri. . . Kama vile unavyopakia behewa, unapoanza kupakia behewa, nilikuwa nikifanya kazi kwenye reli, nasi tungepakia behewa vitu mbalimbali, lakini mkaguzi anakuja kwanza, halina budi kupitia kwenye barabara nyingi mbovu, kama kuna kitu chochote kilicholegea, hatalitia muhuri, mpaka gari hilo limepakiwa *sana* na kushindiliwa sana hata hakuna kitu kinachoweza kulitikisa, ndipo anafunga mlango na kulitia muhuri, wala haliwezi kufunguliwa mpaka lifike kikomo wake. Hiyo ni kweli kabisa.

21 Mungu akija na kupata upumbavu mwingi sana ndani yetu, kamwe Yeye halitii tu muhuri bado, anaona kutokuamini kwingi, Yeye halitii tu muhuri bado, lakini wakati limejazwa na Injili yote, ndipo Yeye analitia muhuri, hiyo ni kweli, analitia muhuri mpaka Kikomo chake. Yeye si ni wa ajabu?

22 Nina furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba mimi ni mmoja wenu. Nami, nilipokuwa mvulana, daima nilitaka watu wanipende, nilikuwa mtu asiyependeka, nilikuwa kwa namna fulani kama yule anayeitwa kondoo mweusi katika familia. Wote walikunywa pombe, mwajua, lakini mimi daima, kama mlivyosoma hadithi ya maisha yangu, hapana shaka, kulikuwa na kitu kilichoniambia kulikuwa na Mungu mahali fulani, mahali fulani, kwamba ningeendelea kusikia Sauti na Kitu fulani kikiniita.

23 Na katika familia kwa namna fulani nilikuwa mtu aliyetengwa na jamii, nilienda shuleni, kwa njia ile ile, maana nilikuwa mshamba sana kila mtu alinidhihaki. Ndipo nilipofanyika mhudumu, niliamini ya kwamba Neno hilo lilikuwa ni Kweli, halafu nilikuwa mtu aliyetengwa na jamii katika kanisa langu la Kibaptisti, walisema, "Utakuwa mtakatifu anayejibingirisha baadhi ya siku hizi." Mnaona? Kwa hiyo basi nilipopata kujua kulikuwa na mtu aliyeyaamini yote kama nilivyoamini, ilikuwa ni kama tu kuweka glavu mkononi, ikatoshea kikamilifu. Kwa hiyo basi, Yeye alisema, "Kama utaacha yote na kunifuata Mimi, nitakupa mama, baba, ndugu, dada," na kadhalika, "na Uzima wa Milele." Kwa hiyo mimi kuja miongoni mwenu namna hii, ninawapenda.

24 Sasa, wakati mwingine ninahubiri kwa ukali sana kwa sababu ni—ninaona hiyo ni, mtu fulani akitoka nje ya mstari, mnaona, unapaswa kufanya hivyo. Baba halisi, mbona, angekutikisa na kusema, "Hima, rudi hapa mstarini," kama yeye

ni baba halisi, wa kweli. Kwa hiyo wakati mwingine mchungaji wenu hana budi kukanyaga kitu fulani, mpendeni tu zaidi hivyo, kwa sababu yeye ni baba halisi kwenu, mnaona, akijaribu kuwaweka sawa, kwa sababu anailinda nafsi yako, ambapo Roho Mtakatifu amemfanya mwangalizi wa kanisa. Na lazima daima uangalie hilo.

25 Ninaomba ya kwamba Mungu atalibariki kanisa hili dogo, na ajalie likue na kufanikiwa, jalia wahubiri wengi wazuri watoke kwenye kanisa hili na waende hudumani kila mahali, jalia jina lake lidumu, ndilo ombi langu. Mungu na ambariki mchungaji wake, mashemasi wake, wadhamini wake, na ushirikishwaji wake, chochote kile, Mungu na awe pamoja nanyi nyote, na washiriki wake wote, mnapojitahidi na kufanya kazi pamoja. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatenda kazi pamoja nanyi, akilithibitisha Neno kwa ishara kuu na maajabu kuwafuata waaminio wanaoliamini Neno, ambalo limehubiriwa kote kwenye jukwaa hili hapa. Mungu awabariki.

26 Sasa, kidogo nimepwelewa na sauti. Ndugu Williams ndiyo kwanza anichanue. Nilimwambia nilikuwa nayo, na nilikuwa nikienda huko Ajo na miji michache kesho. Ninajaribu kutafuta mahali pa kuhamia, huku Arizona, kuishi huku. Halafu katika kuja Arizona, nisingekuja. . .Basi ndugu wa thamani, hivi majuzi asubuhi, baada ya mimi kuhubiri juu ya *Uzao Wa Kifalme*. . .Sasa, mimi si mwuza kanda, nyote mnajua hilo, lakini mvulana huyu hapa anayo hiyo kanda. Sasa, mtu yeyote aliye na kinasasauti, laiti, kama unaweza, upate kanda hiyo ya *Uzao Wa Kifalme*, ya Jumapili iliyopita asubuhi.

27 Naye Ndugu Fuller, alitoka, alitoka akaenda mimbarani baada ya mimi kuondoka, na kuwaambia watu waniambie, nije, nilichukue kanisa lake, yeye na mke wake wangekuwa bawabu. Vema, hilo lilikuwa tamu sana. Ndugu—Ndugu John Sharrit pamoja na kanisa lake, hao watu. . .Lakini sininii. . .mimi, kama ningekuja Phoenix, la, bwana, nisingeanzisha kanisa lolote. La, bwana. Hilo haliko ndani yangu, unaona, maana ukianzisha kanisa, wewe ni. . .

28 Mnaona, si wazo langu kuanzisha kanisa, ni kusaidia yale ambayo tayari yameanzishwa, mnaona. Kama nikija Phoenix, mimi ni mmishenari, ninaingia na kutoka kote ulimwenguni, wakati wote, Ningeninii, mchungaji akinialika, ningekuwa hapa Jumapili moja kumsaidia, halafu Jumapili ijayo kumsaidia jamaa huyo mwingine, na Jumapili ijayo kule kumsaidia jamaa huyo mwingine, kila mahali tu niwezapo ku—kusaidia, na kulifanya zuri kwa kila mtu, mnaona, madhehebu yote na kila kitu, kufanya ushirika.

29 Nami huenda-. . .daima nilitaka kuja magharibi, nami, labda. . .Kifungo cha mwisho kilichonifunga mashariki kilikuwa ni mama yangu ambaye ndio kwanza aende Nyumbani

kuwa pamoja na Yesu majuma machache yaliyopita, na mama wa mke wangu yapata mwaka mmoja uliopita. Kwa hiyo sasa sote wawili ni mayatima, bila baba wala mama katika dunia hii, wametuacha wakaenda kuwa pamoja na Bwana wetu. Nasi tunapanga, labda, Bwana akipenda, kuja magharibi kuishi. Mtuombee.

30 Sasa, sasa, katika, kabla hatujalikaribia Neno. . .Ninataka kusoma baadhi ya Neno, usiku wa leo, na kuzungumza tu kwa muda kidogo. Na jambo lingine, nilisahau, hivi Billy aligawa kadi zozote za maombi? Aligawa, naam. Vema, Bwana. Hilo—hilo ni zuri. Basi tutaninii. . .Patakuwa mahali padogo kwa ajili ya mkutano wa maombi, lakini nimekuwa nao ambapo, mtu fulani alisema, wengine, pamoja, kama vile mchungaji wakati mmoja, wakati mwingine wanapokuwa na kanisa dogo, labda linaloenea watu mia moja ama mia mbili, wanasema, "Loo, Ndugu Branham, kanisa langu lilikuwa kubwa tu vya kutosha!" Ni kubwa mno, Kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni Neno tu kutoka kwa Mungu, unaona, hivyo tu, haidhuru liko wapi.

31 Kamwe siachi mikutano yangu iwe mikubwa, kwa sababu unapofanya hivyo, ama wajibu fulani wa redio, televisheni, ama chochote kile, ama vitabu fulani, ama magazeti, ama kitu fulani, unapofanya hivyo, papo hapo unajifunga mwenyewe. Ninataka kuwa mahali ambapo si lazima niwe na pesa zozote, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu. Na si—sio lazima niwe na pesa, wala mahali hapawezi kuwa padogo kupita kiasi, kama ni katika mkutano wa maombi katika nyumba ndogo ya mashambani, hilo ni sawa.

32 Nilifanya uamsho, hivi majuzi tu, ambapo kanisa, lilijaa kabisa, likaketi watu ishirini, hiyo ni kweli, watu ishirini. Sasa, kama ningalikuwa na kitu kikubwa—kitu kikubwa mno, labda inibidi kuwa na dola elfu kadhaa kwa siku, nisingeweza kwenda mahali kama hapo na kufanya hivyo, mnaona. Lakini ninaamini katika kuongozwa na Roho Mtakatifu, popote anapokuongoza, haidhuru.

33 Halafu nimeenda ng'ambo, huko Bombay, India, nikawahubiria laki tano kwa wakati mmoja, Afrika Kusini, laki mbili ama tatu, huko mbali sana, msininii. . .Mwasema, "Unapataje pesa za kufanya hivyo?" Vema, kama Mungu akinituma, daima Yeye humtuma mtu aliye na pesa, mnaona, kwa hiyo Yeye ni. . .Hatuna budi kuishi kwa imani, mwajua. Kwa hiyo ni maisha mazuri sana, maisha ya imani, sivyo? Mwamini tu Yeye.

34 Na—nami ninasema baadhi ya mikutano bora sana niliyowahi kuwa nayo imekuwa ni makanisa madogo sana kuliko hili, na hiyo ni kweli, ambapo tunakusanyika tu pamoja na kufanya ushirika, kisha Roho Mtakatifu anashuka, na hapo

ndipo Uhai unapozaliwa. Uh-huh. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, bila shaka ni kweli.

35 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kama, kabla hatujalikaribia Neno Lake. Kwa uchaji sasa, baada ya kujisikia kama kwamba tumefahamiana na kwa namna fulani tukajuana, kama kuna ombi hapa, usiku wa leo, ambalo ungetaka nikuombee, la *jambo fulani,* tafadhali inua tu kichwa chako, ama, mkono wako, hasa, na kusema, "Ndugu Branham, niombee." Mungu awabariki. Kila mahali tu, Baba wa Mbinguni anaona.

36 Sasa, Bwana wa thamani, Mungu Mwenyezi, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Aliyewafufua Wafu tena alipomfufua Yesu Kristo katika wafu tuna furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba Yeye alifufuka katika wafu, wala hajafa tena, bali yu hai milele. Miaka elfu mbili imekuja na kupita, na hata hivyo tu—tuko pamoja Naye usiku wa leo, halisi tu kama alivyotembea Galilaya katika siku Zake. Tunajua tu kwamba Yeye amefufuka katika wafu, akijitambulisha Mwenyewe kwetu katika umbo la Roho Mtakatifu, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, Bwana.

37 Na kuona, sasa hivi, katika siku hii ovu tunayoishi, wakati wasioamini na—na wanasayansi, na kadhalika wanapojaribu kukatilia mbali thamani yenyewe ya Neno, hata hivyo Mungu anaishi katika Neno Lake. Nasi tunamwona akijidhihirisha Mwenyewe, akijitambulisha Mwenyewe dhahiri tu na waziwazi kwetu, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, Bwana. Na kujua . . . Vipi kama tungalikuwa nje usiku wa leo, nje ya Safina, wala hatukujua mahali tulipokuwa, nafsi zinazotangatanga kama yule kunguru aliyefunguliwa akatoka kwenye safina? Aliridhika na kuishi juu ya mizoga iliyokufa iliyokuwa bado ikielea juu ya maji bado. Lakini kama vile ilivyombidi maskini yule hua kutafuta njia ya kurudi kwenye safina na kubisha mlango, ama, dirisha, mpaka Baba Nuhu alipomfungulia, basi tuna furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba Baba Mungu ameturuhusu kuingia katika Safina hii.

38 Na, usiku wa leo, tuko salama, tumepumzika kabisa katika upatanisho ambao Bwana wetu alitufanyia, tukijua jambo hili, ya kwamba hukumu zitakapokuja, kwamba tutaelea juu ya hukumu. Tutaondolewa ulimwenguni na hatutalazimika kusimama Hukumuni, kwa kuwa Bwana wetu alituahidi katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

39 Sio nafsi inayotangatanga tunapokufa, tuko katika Uwepo wa Mungu. Si kutangatanga katika Umilele usio na mwisho, tumepotea, kujua inatubidi kurudi na kuhukumiwa kulingana

na matendo yaliyofanywa katika mwili, lakini, Baba, usiku wa leo tumemalizana na hayo madhabahuni, nazo dhambi zetu zimetutangulia, na tumehesabiwa haki kwa Damu ya Yesu Kristo, pamoja na thibitisho lake, Mungu alitumwagia tena Roho Mtakatifu juu yetu, nasi tumetiwa muhuri sasa hata Kikomo chetu cha Milele.

40 Tuna mahitaji, Bwana, tunapopitia ulimwenguni, mwili huu ungali ni wa kawaida, ungali umezaliwa na dhambi, siku moja utazaliwa na Mungu, bali leo hii umezaliwa kwa dhambi. Nasi tunapambana tunapotembea katika ulimwengu huu wenye giza, wenye huzuni, tukiangalia Juu ambapo Nuru pekee ndiyo inayoweza kutokea. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamkumbuka kila mmoja wa watu hao walioinua mikono yao, kuanzia aliye mdogo sana hata aliye mkubwa kuliko wote, kuanzia aliye mchanga sana hata aliye mkubwa kuliko wote, ujibu, Baba, naomba ya kwamba Wewe utawajalia haja zao.

41 Na sasa, tunapofungua kurasa za hiki Kitabu, mtu yeyote anayeweza, aliye na nguvu za kimwili anaweza kufungua hizi kurasa, bali hakuna mtu anayeweza kukifungua ila Yeye aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Tunaona kile Kitabu kimechukuliwa katika mkono Wake yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi. Mwana-kondoo aliweza kukitwaa na kukifungua kile Kitabu na kuifungua mihuri yake, kwa hiyo tunaomba, Mwana-kondoo Mkuu wa Mungu, njoo miongoni mwetu, usiku wa leo, tunapolisoma Neno, kifungulie mioyo yetu kutupa imani kwa ajili ya safari iliyo mbele. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

42 Sasa, watu wengi hupenda kusoma somo na kadhalika, tunapolisoma, nami niliandika mafungu fulani na kadhalika, kama kawaida. Na, usiku wa leo, nataka tufungue Waamuzi, mlango wa 6, na kusoma kwa dakika chache. Na kesho usiku kukiwa ndiko mwanzo wa mkutano, ni—nitajaribu kutowaweka ila kwa muda kidogo tu usiku wa leo, ndipo tutawaombea tu wagonjwa, kisha tuahirishe, na kujiweka tayari kwa ajili ya kesho usiku. Wengine wamesimama, nami ninajua ni vigumu kusimama.

43 Nilipeleka gari langu likatiwe grisi alasiri ya leo, huyo mvulana alikuwa mwenda pole sana ilichukua karibu saa tatu. Basi ni—nilikuwa nikivuna, nadhani kwa yale nimekuwa nikipanda, kwa kuwafanya watu wasimame kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo nikaanza kulalamika, halafu nikanyamaza tu nilipoliwazia, kwa hiyo nikawazia, "La, wamekuwa, wamefanya, kamwe hawakusema chochote, wala sitasema. Kwa hiyo nikaachilia tu."

*Malaika wa Bwana akamtokea, akamwambia, Bwana yu pamoja nawe, ewe shujaa.*

*Gideoni akamwambia, Ee Bwana wangu, ikiwa* BWANA *yu pamoja nasi,...basi...mbona mambo yote haya...yametupata?...yako wapi natendo yake ya ajabu, waliyotuhadithia baba zetu, wakisema, Je, siye* BWANA, *aliyetuleta huku* kutoka *Misri? ila sasa* BWANA *ametutupa, naye ametutia katika mikono ya Wamidiani.*

BWANA *akamtazama, akasema, Enenda kwa uwezo wako huu, nawe utawaokoa Israeli na mikono ya Wamidiani: je, si mimi niliyekutuma?*

44 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Maneno haya. Sasa, sote tunayafahamu Maandiko ambayo ndiyo kwanza nisome, wote, wasomao Biblia. Ulikuwa ni wakati wa waamuzi, ambapo kulikuwa na, vema, kwa namna fulani wakati wa katikati, kutoka kwa wafalme, Mungu amekuwa na waamuzi, na kulikuwako na waamuzi kadhaa. Na kila wakati ambapo ninii...Mungu angewanyosha watu, wote wangejaribu ku—kuanza kutenda haki baada ya Yeye kutuma hukumu ama kitu fulani, ndipo basi muda si muda, wangeanguka tena. Ni kawaida tu kwa watu kufanya hivyo, ni jambo la kibinadamu tu kwao kufanya hivyo, kuanguka. Na—na mara wanapoanguka, ndipo hukumu ya Mungu inapoingia moja kwa moja tena. Mnaona? Huwezi kufanya mabaya na uendelee tu, maana Mungu ni mwenye haki.

45 Sasa, Yeye ana-...Yeye, ili awe mwenye haki, hana budi—hana budi kutimiza sheria Zake, na sheria bila adhabu sio sheria. Mnaona? Kama kuna ba—bango elekezi hapa nje mtaani, nayo inasema "Simama," hiyo ni sheria kwako ya kusimama, ndipo basi kama ukilipita hilo nayo hiyo sheria haina adhabu, basi si sheria tena, unaona, hata halipaswi kutundikwa pale.

46 Na kama Mungu akianza kutikisa kitu mbele yako na kukwambia ya kwamba unafanya makosa, nawe uvunje sheria hiyo ya Mungu inayokuonya, basi adhabu inafaa kulipwa, huna budi kufanya hivyo. Huna budi kufanya hivyo, huna budi kulipia hiyo adhabu. "Na mshahara wa dhambi ni mauti." Kwa hiyo kama mtu akivunja sheria ya Mungu na aendelee kufanya hivyo, basi usimlaumu Mungu kama jambo fulani likikupata. Unaona? Kama umepotea, huwezi kusema, "Vema, ilikuwa ni kosa la Mungu."

47 Mara nyingi nimesema jambo hili, ya kwamba mtu hana budi kujitahidi sana apate kuingia kuzimu, hawezi kwenda kuzimu kirahisi. La, ana wakati mgumu kuingia kuzimu, lakini bila shaka anang'ang'ana kuingia mle.

48 Mnakumbuka, enyi wavulana, maskini sigara ndogo ya kwanza ya gunzi la mahindi uliyovuta? Mnajua nini? Mama akasema, unajua, ulihofu Mama yako angesikia harufu hiyo kwenye pumzi yako, kwa hiyo ulichukua kahawa kidogo

ukaitafuna, ama kitu fulani pale, wajua, isije—isije ikanuswa, Mama akasema, "Hebu nisikie harufu ya pumzi yako." Unaona?

"Mama, sina shida yoyote."

49 Jambo la kwanza ni lipi? Wakati uliposema uongo huo wa kwanza, taa nyekundu ilianza kumulika, "Mwambie ukweli. Kuwa mwaminifu, ewe mvulana mdogo, Mama alikufundisha kufanya hivyo." Lakini, unaona, unang'ang'ania kupenya kizuizi hicho pamoja na taa nyekundu. Unaona?

50 Unakumbuka mara ya kwanza ulipomchezea rafiki yako wa kike? Um-hum. Unakumbuka mara ya kwanza ulipo—ulipomjibu vibaya mkeo, mke alipomjibu vibaya mumewe, ama kitu kama hicho? Unakumbuka mara ya kwanza uliposikia wimbo huo ukiimbwa kanisani na Kitu fulani kikapiga moyoni mwako, nawe ukajitikisa tu na kuondoka? "Nitafanya hivyo wakati mwingine."

51 Hizo zote ni taa nyekundu, mnaona, mnaona, nanyi mnatembea tu moja kwa moja juu yake, maonyo, "Usiende jinsi unavyoenda ewe mvulana mdogo, msichana mdogo, nirudie Mimi, Mimi ndiye Muumba wako," bali unaipita moja kwa moja.

52 Huwezi kutarajia kitu kingine, usimlaumu Mungu. Ukiipita taa hiyo ya kusimamisha huko nje usiseme, "Mamlaka ya jiji ndio wa kulaumiwa." La, bwana, aliyekosea ni wewe. Taa hiyo ya kusimamisha imewekwa kukulinda, na kukusaidia, nawe huna budi kuitii. Ndipo basi si kosa la mamlaka ya Jiji, ni kosa lako, maana ulipaswa kusimama wakati onyo lilipotolewa.

53 Basi unapouhisi huo mlio mdogo moyoni mwako ukikuonya, basi afadhali usimame papo hapo na kufanya hesabu. Kama nilivyokuwa, nimekuwa nikihubiri usiku mzima juu ya watu kumwacha Mungu, unapolisikia Neno, rudi moja kwa moja, kwenye Neno la Mungu kweli. Kuna kengele ndogo inayolia, heri uisikilize. Um-hum. Sasa, usipite hiyo, maana kamwe hutaweza kuendelea mbele zaidi mpaka utakaporudi moja kwa moja hapa ulipomwachia.

54 Utaninii . . . Unapomwachia Kristo, kwa kukosa kulitii Neno Lake, papo hapo Yeye atakuacha, ama, huachi- . . . Yeye hakuachi, wewe unamwacha. Unaona, daima una—unamwacha Yeye, kwa sababu amekuweka njiani, Yeye anajaribu kukuongoza, lakini unaona, unapomwacha, basi huna budi kurudi moja kwa moja mahali ulipomwachia, kuanza tena.

55 Nilikuwa na rafiki kasisi aliyekuwa akinisimulia kisa fulani katika Vita vya Pili vya Dunia. Kulikuwako na ka—kapteni aliyekuwa amepigwa risasi kwa ninii—ninii, nadhani bombomu ya aina ya takriban .50 hivi, alikatwa kifuani mwake, naye alikuwa—alikuwa yuafa. Naye akaitiwa huyu kasisi, walimwambia atoke aende hemani, walikuwa ndio kwanza wamwokote, katika hema la hospitalini, kwamba alikuwa yuafa.

Asingeweza kuishi, tayari alikuwa amekatwakatwa kwa risasi na asingeweza kuishi, alikuwa akitokwa na damu kwa ndani.

Na kwa hiyo, kasisi akasema alifika kwa mtu huyo, mahali alipokuwa, naye akasema, "Kapteni, wewe—wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Nilikuwa."

Naye akasema, "Ati ulikuwa?" Kasema, "Mbona, unapaswa kuwa sasa, kwa sababu unajua unakufa."

Akasema, "Naam, bwana, ninajua hilo."

56 Akasema, "Sasa, Kapteni, sasa tafakari nyuma kwa yote, sasa, afadhali utafakari upesi maana huna muda mwingi, bali yatafakari ya nyuma, huko nyuma kabisa, mahali ulipomwacha Kristo, na papo hapo ulipomwacha Kristo, basi anzia papo hapo, na uanzie papo hapo, maana utampata pale pale ulipomwacha."

57 Sasa, huenda ulimwacha kwenye—kwenye Fu—Fundisho katika Biblia, Kitu kilichokwambia, "Usiibe," ukaipita moja kwa moja, "Usiseme uongo," ukaipita moja kwa moja, *jambo lingine* ambalo hukupaswa kufanya, na hata hivyo ukalipita moja kwa moja, sasa, itakubidi kurudi moja kwa moja na kulichukulia papo hapo tena.

58 Na kwa hiyo, kapteni huyu alikuwa akitokwa na damu kwa ndani, huku damu ikitiririka mapafuni mwake, naye alikuwa akivuta pumzi upesi sana, naye alijua alikuwa anaondoka. Kasema, "Afadhali uharakishe, Kapteni, na utafakari."

Akasema, "Sikumbuki kabisa." Ndipo baada ya kitambo kidogo nuru ikaja juu ya uso wake, akasema, "Ninakumbuka, ninakumbuka pale pale nilipomwacha."

Kasema, "Vema, Kapteni, anzia papo hapo."

59 Naye akasema:

> Sasa najilaza nipate kulala usingizi,
> Naomba Bwana ailinde nafsi yangu;
> Na kama nikifa kabla sijaamka,
> Ninaomba Bwana nafsi yangu aichukue.

60 Naye akaanguka pale. Alimwacha Kristo wapi? Utotoni, mnaona, miguuni mwa mama, mnaona, kama mvulana mdogo. Ilimbidi kurudi huko nyuma kabisa kumchukua. Hapo ndipo utakapomchukulia, mahali ulipomwacha.

61 Israeli, daima wakitoka kwenye upatanifu wa Mungu; hakuna kitu kinachoenda sawa mpaka urudi kwenye upatanifu wa Mungu. Na sasa, walikuwa ndio kwanza wakombolewe kutoka kwenye je—jeshi la kigeni, na badala ya kumgeukia Bwana, waligeuka moja kwa moja wakamwacha tena.

62 Si inashangaza? Tutashikwa na ugonjwa, mtoto atakuwa mgonjwa sana hata hatujui la kufanya. Mama ataikunja mikono yake, naye Baba atasema, "Ee Mungu, tutakutumikia kama utamponya tu mtoto huyu mchanga." Ndipo huyo mtoto

mchanga anapata afya, halafu unasahau jambo hilo. Unaona? Unaona? Ni rahisi sana kusahau hilo. Naam, bwana.

63 Kisha utaona ajali ambayo karibu iyachukue maisha yako nawe utasema, "Loo, kama ningalikufa! Bwana, asante kwa kuniokoa, nitakutumikia Wewe." Kisha unasahau jambo hilo, unaona, mpaka moja ikupate, unaona, ndipo basi—ndipo imechelewa sana. Unaona, wewe—wewe daima, watu kwa kawaida humsahau Mungu, hawafanyi hivyo daima, Mungu ashukuriwe kwa ajili ya jambo hilo, lakini, mara nyingi, ni rahisi sana kusahau wakati kila kitu kinaendelea vizuri.

64 Halafu, mwajua, Yeye alisema kama ungempuuza, wala usimtumikie, basi msiba wako utakapokuja Yeye angekucheka tu, unaona. Kwa hiyo lazima ukumbuke, hatuna budi kumweka Mungu kwanza, sikuzote.

65 Sasa, watu walikuwa wamemwacha Mungu nao walikuwa wamekosea, na kwa hiyo Wamidiani, na Wafilisti, na mataifa mbalimbali wangeingia na kuwateka.

66 Sasa, hatuna Wamidiani na Wafilisti, lakini tuna wabaya zaidi, ulimwengu unaingia moja kwa moja, unatula, unatushusha tu chini, mnaona, kutokuamini. Nasi tunaondoka moja kwa moja kutoka kwenye sehemu ya Roho ya Kanisa, na sehemu ya Roho ya Mungu, tunaenda kwenye mambo ya kawaida, na kuninii tu, "U hali gani, Mchungaji? Ninataka kuhamisha barua yangu kutoka kwenye kanisa *hili* hapa, kwa sababu wao, Dada *Nanii*, mimi na yeye hatuzungumziani, kwa hiyo nitaileta nyumbani kwako." Mnaona? Haya basi. Loo, naam, mnaona. Halafu basi, hapo, mnaona, tunapitisha tu barua. Lakini ukiisha kuliandika kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, liko Nyumbani basi. Unaona? Hiyo ni kweli.

67 Sasa, lakini tunaona ya kwamba mambo haya yanatukia. Basi wa—wakati ulikuwa umewadia, katika jambo hili, wa kutenda kazi, kwa sababu Wamidiani walikuwa wamekuja kama nzige kote nchini. Ndipo ikawabidi Waisraeli kuchimba mapango milimani wapate kujificha, warudi mle ndani na kuficha chakula kidogo wapate kuishi, wakirudi tu, huko nyuma kabisa, wawaondokee, kwa sababu, mbona, walikuwa wanaingia, umati wao tu.

68 Wangewaleta kondoo wao, mifugo yao, maksai wao, na kula kila kitu ambacho Waisraeli walikuwa wamepanda, mazao yao yote na kadhalika namna hiyo, na kuwafukuza, kwa hiyo walikuwa—walikuwa wanaenda kuwaondoa, na kwa hiyo, wakala walichokuwa nacho. Hawangewaua, wangewaacha warudi mwaka ujao na kupanda mazao, yapata wakati mazao yalipoiva, huyu hapa anaingia tena, ayatwae.

69 Kwa hiyo tunaona ya kwamba kulikuwa na mtu shujaa, ambaye kweli hakudai kuwa hivyo, bali alikuwa akipepeta ngano yake karibu na shinikizo la zabibu, akijaribu kuitia

kidogo pamoja kuishughulikia familia yake kwa mwaka huo, jina lake lilikuwa Gideoni, baadaye akawa mwamuzi katika Israeli.

70 Sasa, tunaona ya kwamba kabla Mungu hajatuma ukombozi kwa watu Wake, sasa, ninawatakeni mshike jambo hili sasa, kwa yale yatakayofuata baadaye, kabla Mungu hajatuma ukombozi kwa watu Wake daima Yeye humtuma nabii kuwajulisha, daima huwatuma manabii Wake, kwa sababu, mara nyingi, watu hawatasoma na kujifunza Neno Lake, kwa urahisi wanaenda tu kujiunga na kanisa, na hilo latosha, hawaketi chini na kusoma.

71 Roho Mtakatifu, Yeye hula Neno la Mungu. Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Kwa hiyo unapookoka, jambo bora zaidi la kufanya ni kuketi pamoja na Biblia yako, soma sikuzote, hiyo inakujenga, unaona kile Mungu alichofanya. Si kama kusoma riwaya fulani, unasoma ili uweze kushikisha nafsi yako kwenye kila alama za uakifishaji ndani Yake, hiyo ni kweli, kwa sababu ni Neno la Mungu, mnaona.

72 Kila wakati Mungu anaposema jambo lolote, mnajua jinsi ninavyoliitikia? Kwa "Amina." Hiyo ni kweli. "Na iwe hivyo." Hiyo ni kweli. Yale aliyosema ni kweli, na kwa hiyo tunapaswa kuitikia Maneno yote ya Mungu kwa, "Amina." Mungu anaposema, "Utafanya," "Usifanye," na kadhalika, sema, "Amina. Amina." Sio kusema, "Vema, ninaamini inapaswa kuwa *hivi*." Sema tu, "Amina," kwa yale Yeye asemayo, hilo—hilo linatosha.

73 Kwa hiyo basi, Mungu alikuwa—alikuwa mwema kwao, nao—nao hawakuwa wamestahili jambo hilo. Lakini basi, kabla ya tukio hili kuu kutukia, tunaona ya kwamba nabii alitumwa kwao, naye akanena Neno la Bwana kwa ajili Yake. Na ndipo tunaona mara baada ya Ujumbe wa nabii huyo, wakati alipowajia Israeli, na kusema, "Mimi ndimi Mungu niliyewapandisha kutoka Misri. Mimi Ndimi niliyewapa nchi mnayoishi, na nimewafanyia mambo haya yote."

74 Mnaona, nabii daima huelekeza nyuma kwa Mungu mkuu, wa kimbinguni, nabii halisi wa Mungu, ambaye ni mhubiri halisi, mimbarani. Na—nabii wa siku hizi ni—ni mhubiri, kwa hiyo nabii halisi wa kweli huelekeza nyuma kwenye Neno la Bwana, ahadi ya Bwana, si lile tangazo ka—kanisa limetoa, bali ta—tangazo ambalo Mungu ametoa. Mnaona? Rudini kwenye Neno la Bwana.

75 Kwa hiyo Mungu alinena na nabii huyu, nao, Wamidiani wamechukua yote waliyokuwa nayo, nao walikuwa wakifa kwa njaa, Naye akasema, "Hivi hamkumbuki ya kwamba Mimi ndimi Mungu niliyewapandisha kutoka Misri? Hivi hamjui ya kwamba nilifanya miujiza Yangu yote huko chini Misri? Hivi hamjui niliifungua Bahari ya Shamu? Niliwalisha baba zenu

kwa muda wa miaka arobaini nyikani, niliwavunja-vunja adui waliowazunguka. Sikuwaangamiza Waamaleki na kadhalika mbele zenu? Mimi ni Mungu, nirudieni tu, niangalieni."

76 Basi kumbukeni, daima, ama, mara baada ya Ujumbe huo wa nabii, Mungu anaingia kazini. Baada ya nabii kutoa Neno, ndipo Mungu huanza kutenda kazi juu ya Neno. Kwanza, halina budi kutokea kwanza, Neno halina budi kuhubiriwa kwanza, "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Nabii wa kweli husimama na Neno la kweli la Mungu wala hapatani juu Yake kwa njia yoyote, bali anawaambia watu kwamba "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie," kama yeye ni nabii wa kweli.

Kama sivyo, atasema, "Vema, sasa, tunaamini ya kwamba . . . "

77 "Sisi" ni akina nani? Si Mungu na manabii Wake, na Mungu na Malaika Zake, na Mungu na Neno Lake. Wanasema ya kwamba "Mbingu na nchi zitapita," alisema Yesu, "bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Hiyo ni kweli. "Mtu yeyote akiongeza kwake, ama kuondoa lolote la Maneno ya unabii wa Kitabu hiki, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima." Kwa hiyo mnaona, nabii halisi wa kweli hudumu na Neno.

78 Basi akaanza kuwaonyesha yaliyokuwa yakitukia. Mara Mungu akajitokeza jukwaani, mara baada ya Ujumbe wa huyo nabii. Daima imekuwa hivyo, kwamba Mungu, sasa kumbukeni, Mungu huenda nyuma ya nabii kama huyo nabii ana Neno la Mungu, "Kwa maana Neno Langu halitanirudia bure, bali litatimiza yale liliyotumiwa, kusudi lililotumiwa."

79 Itabidi lije, kutakuwako na kundi ambalo litaninii tu, kama kutupa maji mgongoni mwa bata, bali kutakuwako na mtu fulani kule atakayelipata kwa sababu Mungu analituma. Amina. Vema. Mnaona? Neno halitarudi bure, litatimiza kile lilichokusudiwa.

80 Na sasa, nabii huyu alisimama na kutabiri. Sababu ya Mungu kumtuma nabii, watu wanaenda mbali sana na Mungu kwa mapokeo ya wazee na kadhalika, nao wanaingiza kanisani kila kitu ambacho ni cha kilimwengu, na muda si muda mwajua wanapatana kidogo *hapa* na kidogo *pale*, na kidogo *hapa* na kidogo *pale*, na muda si muda mwajua si kitu ila dhehebu, si chochote bali kama chama.

81 Watu huja pale na wana—wana supu za kila namna, na dansi, na kucheza karata, na kadhalika kanisani, na si zaidi ya—ya chama. Hiyo ni kweli. Lakini basi, mnaona basi hiyo ni mbali sana na Neno. Na watu wengi waaminifu wanaketi katika vyumba hivyo vikubwa vya maiti huko nje na kuwazia, "Hili *ndilo*."

82 Na kabla Mungu hajatuma Hukumu Yake, kabla hajaruhusu jambo lolote litendeke, kabla ya ukombozi kuja kwa ajili ya

Kanisa, Mungu ni mwenye haki Naye hutuma Sauti kote nchini ikinena Neno la Bwana Mungu. Ndipo mara Mungu anaponena Neno Lake, Mungu yuko katika Neno Lake kulifanya halisi na kulidhihirisha Neno Lake yale aliyosema.

83 Mungu ni mwenye haki, kamwe hawezi kuwa kitu kingine ila Mungu mwenye haki. Mnaona? Yeye husimama moja kwa moja nyuma ya Neno Lake. Wakati Neno hilo la kweli linapotolewa, Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Kwa sababu ni Neno la Mungu, halina budi kutokea.

84 Sasa, vipi. . .? Mungu hashuki na kulinena dhahiri kwa Sauti Yake kutoka Mbinguni, Yeye ameliandika kwenye karatasi huku akinitarajia mimi na wewe kumpokea Roho Mtakatifu, tupate kuliamini Neno hilo. Nasi tunaponena Neno hilo, kama ni Neno la kweli la Mungu, Mungu husimama nyuma Yake. Hiyo ni kweli. Mungu hufanya miujiza kupitia mikono ya watoto Wake.

85 Kama nilivyosema hapa siku chache zilizopita usiku katika kanisa fulani, Yeye ni Mzabibu nasi ni matawi. Mzabibu hauzai tunda, matawi ndiyo yanayozaa tunda, bali hupata nguvu zake kutoka kwa mzabibu. Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, huingia katika mwili wa mwanadamu, anashika Neno Lake Mwenyewe na kuliondoa, anaonyesha maono, ananena kwa lugha, anatabiri, Yeye hufanya kila namna ya kazi kuthibitisha Neno Lake akimtumia mwanadamu, hivyo ndivyo alivyofanya hasa.

86 "Ninyi ni mashahidi Wangu. Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, na ndipo basi ninyi ni mashahidi Wangu," Mnaona? Hamna budi kurekebisha jambo hilo kwanza. "Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, mpaka mtakapovikwa Nguvu. Ndipo ninyi ni mashahidi Wangu. Katika Yerusalemu pekee." La, "Yerusalemu, Yuda, Samaria, na hata pande za mwisho za ulimwengu, ninyi ni mashahidi Wangu."

87 Baada ya m—m—mzabibu na tawi kuunganishwa pamoja, ama, baada ya mzabibu kuzaa tawi, kwa maana kama mmoja ni wa kupandikizwa, hautazaa tunda linalofaa, bali mzabibu wenyewe ukichipusha tawi, litakuwa, aina ya uhai ulio kwenye tawi utakuwa katika mzabibu ukizaa hilo tunda. Kwa hiyo, nabii wa kweli wa Mungu anasema Neno la Mungu ni sahihi kuanzia A hadi Z, kila Neno Lake, ni kweli.

88 Sasa, sababu ya Mungu kuwafanya watu hao na kuwatuma watu hao, ni kwa sababu kama watu hawatajifunza Biblia, hawatasoma Biblia, hawatasoma, hawataomba, si zaidi ya kuandika maombi mafupi na kuyakariri asubuhi, ama *kitu fulani*, ama kupitia shanga chache, na kukariri *jambo fulani*, na, ama salamu Maria na kuninii tu. . .?. . .kitu fulani, lakini hilo silo. Mnaona? Lakini Mungu humtuma nabii wa kweli, nalo Neno la Bwana humjia nabii, daima. Neno la Bwana humjia nabii.

89 Na basi kama Neno la Bwana liko ndani ya nabii, ndipo basi watu wanaweza kumwona Mungu katika matendo, Neno la Mungu likitenda kazi katika nabii, haya basi, maana Mungu huthibitisha Neno Lake.

90 Mwangalieni Petro, alimwona Mungu akitenda kazi. Mwangalieni Paulo, alimwona Mungu akitenda kazi. Waangalieni manabii wa kale, walimwona Mungu akitenda kazi. Kweli kabisa. Hebu mchukue mtu leo hii, mhubiri anayehubiri Injili yote, ubatizo wa Roho Mtakatifu, watawaangalia hao watu na kumwona Mungu akitenda kazi, atakuwa na maisha ambayo yataakisi mahali popote, yasiyoshutumika, chochote kile. Mnaona? Ni Mungu akitenda kazi ambapo watu wanaweza kuona. "Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa." Ni waraka wa namna gani? Waraka wa Mungu, Mungu akishuhudia ya kwamba Yeye alikutuma.

91 Kwa hiyo tunaona ya kwamba Yeye huwatuma manabii Wake, na wao ndio kitu kinachoangaza na kuwaonyesha watu Injili. Mungu asifiwe, na—napenda hilo. Wakitoka kwenye seminari ya Mbinguni, naam, bwana, huku Mungu akithibitisha ya kwamba wanatoka Huko, si sana sana kujua *ukoo*, bali *elimu-magoti* nyingi ikitekelezwa. Hiyo ni kweli. Sasa, sasa angalieni, sasa, wakati sisi . . .

92 Gideoni, angekuwa katika hali mbaya sana. Alikuwa huko nje akipura ngano yake, na muda si muda mwajua, akaangalia kule . . . Naye alikuwa ndiyo kwanza ausikie Ujumbe wa nabii huyo. Sasa, mtapata hayo katika kifungu cha 7 hadi cha 10, mnaweza kuona mahali alipokutana, na—na—nabii alikuja na kutoa U—Ujumbe, akiwaambia kwamba wakumbuke ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu, na Yeye ni Mungu yeye yule aliyewakomboa, na ili nao wamrudie tu. Sasa, huo si ungekuwa ni Ujumbe wa siku hizi? Jamani, bila shaka ungekuwa.

93 Mungu angali ni Mungu. Mungu ni Mungu aliyekuwa kwenye Pentekoste, Mungu ni Mungu aliyekuwa katika kichaka kilichowaka moto, Mungu ni Mungu aliyeifungua Bahari ya Shamu. Tunajali nini kuhusu mabomu ya haidrojeni, ama makimbilio ya mnururisho, ama chochote cha zaidi mwanadamu anachoweza kutengeneza? "Mungu ndiye Kimbilio letu na Nguvu zetu, Msaada uliopo kabisa wakati wa shida." Yeye angali ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka, Mungu wa Daudi. Bila shaka. Yeye angali ni Mungu. Tunataka tu kusikia Neno, hilo ndilo . . . Tunashukuru ya kwamba tumesikia Neno na kupata kuwa ni kweli. Naam, bwana.

94 Yeye ni Mwamba, Mnara wenye nguvu, Naye ni Kimbilio wakati wa dhoruba, kwa hiyo Yeye ni Kimbilio letu, "Wenye haki wanakimbilia kwenye Ngome hii, wakawa salama." Naam, wako salama, hiyo ni kweli. Yuko kwenye bamba la nyumbani, anaitwa, "Salama!" na Hakimu Mkuu, hiyo ni kweli, kwamba

yuko salama. "Wale wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya." Yeye ndiye Nyumba ya kimbilio.

95 Sasa, Gideoni, wakati alipokuwa huko nje akipura ngano yake, hapana shaka Ujumbe wa nabii huyo ulikuwa ukipitia moyoni mwake, yale nabii huyo aliyosema, "Mimi ni Mungu wa—wa Ibrahimu, Isaka, Yakobo. Mimi Ndimi niliyewatoa Misri. Mimi Ndimi niliyewapa kile mlicho nacho. Nigeukieni Mimi!" Naye huyo hapo yeye na baba yake huko nje wakiipura ngano hii, ndipo Malaika akamjia, ama, alidhani ilikuwa ni Malaika, ilitokea haikuwa ni Malaika, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe, maana mna, angalieni, herufi kubwa za B-W-A-N-A, mnaona.

96 Ndipo alipozungumza na Gideoni, Gideoni alishangaa kidogo, Akasema, "Sasa, ewe shujaa," hakujua alikuwa. Labda hujui ndivyo ulivyo. Nyinyi, huenda mkawa wengi wa hao watu shujaa usiku wa leo, walioketi hapa. Unasema, "Hili—hili kanisa dogo, kundi dogo?" Loo, jamani. Walikuwa wawili tu pale, yeye na baba yake. Inabidi tu kuwe na wawili hapa, wewe na Kristo, hilo tu ndilo linalohitajika kuwa shujaa. Hiyo ni kweli.

97 Sasa, muda si muda mwajua, kilichotukia, mara tu Yeye aliponena na Gideoni, "Ewe shujaa," alimwita, kile alichoweza kufanya.

98 Naye akasema, "La, Bwana, la, Bwana, mimi—mimi ninaninii tu, si—si—siwezi kuamini hilo." Sasa, alionekana kama, labda, mzee mwenye upara, ameketi pale akiegemea kichaka, mwajua, ameketi huko nyuma ameegemea kichaka, labda amejifunika ngozi ya kondoo, ama *kitu fulani,* fimbo mkononi Mwake, hakuvutia sana.

99 Naye akasema, akamwambia alikuwa amekuja kumwagiza aende kuwakomboa Israeli. Huyo nabii alikuwa tayari ametoa Ujumbe wake, kwa hiyo Yeye akasema, "Ninakutuma kufanya jambo hili."

"Mbona," akasema, "La, Bwana, la. La, la. Ninajua huenda nabii alisema *hivi na hivi* na *hivi na vile*, lakini—lakini kumbukeni. . ."

Alisema, "Mungu yu pamoja nawe."

Akasema, "Kama Mungu yu pamoja nasi, basi iko wapi miujiza Yake yote?" Hilo hapo swali.

100 Vema, sasa, vipi kama yeye angalisema, "Loo, hakika, shirika letu lilipata watu elfu kumi mwaka huu, Mungu yu pamoja nasi. La, kila mmoja wetu alifanikiwa sana, kila kitu kilifanikiwa mpaka kila mmoja wetu akapata Kadilaki mbili"? Hivyo ndivyo ninii yako. . .huwezi kuwa wa kiroho siku hizi mpaka umiliki Kadilaki tatu ama nne, mwajua, mlolongo wa vitu vya namna hii, mnaona, kitu kama hicho, uwe na kitu kikubwa kuliko vyote kilichopo nchini.

101 Lakini sikilizeni, la, a—asingeweza kupata hilo, hakusema hivyo, mnaona. Akasema, "Kama. . ." Leo tunasema, "Vema, mnajuaje Mungu yu pamoja nasi? Maana idadi yetu inanaongezeka, tuna makanisa mengi kuliko tuliyowahi kuwa nayo. Tuna. . .Mbona, mwajua, hata meya wa jiji huja kanisani mwetu. Tunajua, sisi—sisi—sisi ndio kanisa kubwa kuliko yote katika. . .sisi ndio bora kuliko wote walioko, tunajua ya kwamba Mungu yu pamoja nasi kwa sababu watu wetu wanafanikiwa, wanavaa nguo bora zaidi, wao ni—wao ni, wana makazi bora zaidi." Hilo ni—hilo ni sawa, tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, bali hiyo si ishara Mungu yu pamoja nanyi.

102 Gideoni alijua alichokuwa akizungumzia, alisema, "Basi, Bwana, kama Mungu yu pamoja nasi, iko wapi miujiza Yake yote mikuu?" Hiyo ni kweli. "Nabii huyo alitwambia ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu aliyetutoa Misri, akaipiga hiyo nchi, akawakomboa, Yeye ni Mungu wa ukombozi. Na kama Yeye alipata kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu."

103 Ninasema jambo lile lile, usiku wa leo: Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye hana budi kubaki Mungu daima. Kama aliwahi kuwa Mwenyezi, Yeye angali ni Mwenyezi, bila shaka ndivyo alivyo. Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

104 Akasema, "Sasa, kama Huyo ni Mungu, kama Mungu yu pamoja nasi, miujiza yote iko wapi? Ziko wapi ishara zote alizofanya?" Sasa, huenda walikuwa na kila namna ya ishara na chochote kile, bali hazikuwa ni ishara za Kimaandiko. Sasa, hu—huna budi kuwa na ishara ya Kimaandiko.

105 Yesu alisema. . .Baadhi yao walisema, "Vema—vema, kama tuna washiriki wengi zaidi, kama tuna dhehebu kubwa zaidi, kama tuna *hili*, *lile*, ama *lingine*, watu waliovalia vizuri zaidi, kama makanisa yetu yanakua, madhehebu yetu, dhehebu letu, wahudumu we—we—wetu wamefunzwa vizuri zaidi, hiyo si ni ishara kwamba Mungu yuko pamoja nasi?" La, bwana, haina uhusiano wowote nalo.

106 Yesu hakusema, "Watakuwa na madhehebu bora zaidi wanapokua na—na kunitumikia Mimi, watakuwa na makanisa bora zaidi wanapokua na kunitumikia Mimi." Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu watatoa pepo, na kunena kwa lugha mpya." Haya basi, hizo ni ishara za Kimaandiko. Naam, bwana. Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi Yeye yuko wapi? Tuna haki ya kusema hivyo.

107 Wakati Elisha alipokuwa amemfuata Eliya, naye akasema, "Nitaomba jambo moja, hilo ni sehemu maradufu ya roho iliyo juu yako," naye akamrushia joho lake, akashuka akaenda kule, akavua hilo joho, akaupiga Yordani, na kusema, "Yuko wapi Mungu wa Eliya?" ukafunguka tena.

108 Basi kama Kanisa leo. . .Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, tuna haki ya kumwita na kusema, "Iko wapi ile—ile ahadi ambayo Yesu Kristo alitoa? 'Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.' Ahadi Yake iko wapi? Jalia nimwone akizitenda kazi Zake."

109 Jambo linalohitajika, ni kwanza, Neno Lake. Usitoke hapa nje kwa hamaki fulani na kuamini unaweza kufanya hivyo, huna budi kurudi kwenye Neno, ufuate masharti vizuri. Inakupasa, huna budi kuliamini Neno Lake, na kutenda kulingana na kila Neno alilosema, upate kuona matendo makuu ya Mungu. Sasa, kumbukeni, kama tu mtafanya hivyo, mnaona, kuliamini Neno Lake, yale aliyosema, na kisha kuyatekeleza. Unaamini hilo?

110 Sasa, huwezi tu kupanda na kupeana mikono na mhudumu, na kuchukua chumvi na kunyunyiziwa maji kidogo juu yako na kusema, "Sasa, yote yamekwisha, wape mkono wa kuume wa ushirika." Hilo si la Kimaandiko. La, hiyo si kweli. Huwezi kufanya hivyo, huna budi kulifuata Neno, huna budi kufanya yale hasa Mungu aliyosema ufanye. Hiyo ni kweli.

111 Huwezi kusema, "Vema, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, ninaamini nilimpokea Roho Mtakatifu nilipoamini." Hivyo sivyo Biblia ilivyosema. La, bwana, sivyo. Unaweza kuamini, ni kweli, hata Uzima wa Milele, lakini basi inakupasa uwe na Mungu apate kulitia muhuri kwa Roho Mtakatifu. "Je, umempokea Roho Mtakatifu *tangu* ulipoamini?" Unaona? Si wakati unapoamini, bali baada ya kuamini unampokea nanii Mtakatifu. . .Baada ya kuamini basi ulitiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi, yasema Maandiko, *baada* ya kuamini. Hiyo ni kweli. Lakini kwanza huna budi kuliamini na kulitekeleza.

112 Huwezi kusema, "Loo," kuna waunga mkono wengi wanaosema, "loo, Biblia ni ya kweli. Naam, Ndugu Branham, ninaamini hilo, Biblia ni sahihi, bali unajua, si—sijui." Haya basi, "*Lakini* mimi," unaona, haya basi, kama tu maskini mbuzi anayegonga kwa kichwa, mwajua, ninii tu, mnaona, "*Lakini*, ni sawa, *lakini* unajua, loo, mchungaji wetu haamini hilo. Ni sawa, *lakini* si—siamini inaweza kutendeka." Mnaona, ha—haya basi tena, mnaona. Kamwe hutaliona likifanywa. Huna budi kutenda, huna budi kufanya jambo fulani.

113 Na wakati utakapochukua ahadi ya Mungu, na kujua ya kwamba ni ahadi ya Mungu, na kuitekeleza, utaona miujiza mikubwa ya Mungu ikirudi kwenye Kanisa la Mungu aliye hai. Hiyo ni kweli, utafanya hivyo.

114 Sasa, wazieni tu jambo hili, enyi marafiki: Mungu angewezaje kusema uongo? Je, utaamini kanisa? Wakati kwa mara ya kwanza. . .Mama ya—yangu alipokuwa akifa hivi majuzi, alisema, alimwambia Delores, huyo ni dada yangu, wavulana tisa na msichana mmoja, Delores alikuwa ndiye

mdogo kuliko wote, alisema, "Delores, wewe ndiwe kitinda mimba changu. Umenipenda, na kunisaidia, ukashuka kuja kunifulia nguo, na kunitunza tangu nimekuwa mzee."

115 Kasema, "Billy, wewe ndiwe kifungua mimba changu." Kasema, "Umenilisha, na kuhakikisha ya kwamba sikuona njaa, na—na huko nyuma kabisa kabla baba yako hajafa, miaka kumi na mitano, ishirini na mitano iliyopita," tena kasema, "daima umenijali, na kuona kwamba nilikuwa na chakula, na mafuta, na kila kitu." Kisha kasema, "Billy, umekuwa kiongozi, kiongozi wa kiroho kwangu ambaye ameniongoza kwa Bwana Yesu." Kisha kasema, "Sasa, leo, ninaenda, nami nina furaha, nataka kwenda Nyumbani sana sijui la kufanya."

116 Sasa, ndipo nikasimama pale, nami nikasema, "Mama, unajua asili yetu ni Katoliki, kwa hiyo nilipokuwa mvulana mdogo na Sauti hiyo ikanena nami, kasema, 'Kamwe usivute sigara, kunywa pombe, wala chochote kile, kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima,' nilishuka kwenda kwenye kanisa Katoliki nipate kujua. Kasisi akasema hivi, akasema, 'Unajua, sisi ndio Kanisa, sisi ndio kundi la watu. Mungu yuko katika Kanisa Lake.'

117 "Vema, basi, nikawazia, 'Si sawa, mengi ya haya mengine, inanibidi kwenda kuona yale hilo lingine liliyosema.' Nikamwendea Mlutheri, wakasema, 'Loo, la, *sisi* ndio Kanisa.' Nikagundua kile *kanisa* lilichokuwa, lilikuwa ni kundi la watu walioitwa watoke. Vema, wao, Walutheri walielekeza njia moja, Katoliki nyingine, Baptisti nyingine, Methodisti nyingine, Presbiteri nyingine, nisingeweza kuweka imani yoyote katika hilo. Kwamba ni lipi, ni lipi Kanisa? Kila moja lilikuwa na kitu kilichosikika sawa.

118 Mwajua, "Mbona," nikasema, "Mama, nilirudi moja kwa moja kwenye Biblia. 'Neno la kila mtu na liwe uongo na Langu kweli.' Nami niliifuata Biblia hiyo yale tu iliyosema, nami nikapata matokeo yale yale waliyopata huko nyuma. Kwa hiyo mimi . . . " Nasi tulikuwa tukitegemea hilo, ni matokeo yale yale. Mungu hana budi kutimiza Neno Lake, hiyo ni sahihi, kweli, kama tu tutaliamini, tulitii, tulikubali, na kulitekeleza.

119 Nuhu alikuwa na ahadi kutoka kwa Mungu, Mungu ndiye aliyenena na Nuhu, lakini Nuhu, kabla hajaweza kuona mwujiza mkuu wa Mungu, ilimbidi aanze kuijenga safina, ilimbidi kujenga safina akishikilia Neno, akiupigilia ubao, akiipiga lami itoke, akiimimina kwenye mbao. Ilimbidi kuitayarisha safina wakati ikisikika ya ukichaa kwa wengine wote. Lakini alikuwa akifanya nini? Akiitayarisha kwa vyovyote vile. Hapana shaka alikuwa akiijenga kwa zaidi ya miaka mia moja na ishirini, akijenga safina, bado hakuna dalili ya kitu kingine chochote, bali alilishikilia Neno, alikuwa akitekeleza agizo lake. Amina. Hmm!

120 "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Tekeleza agizo lako, uone kile Mungu anachofanya. Tekeleza agizo lako. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," Mnaona? Tekeleza agizo lako.

121 Unasema, "Nilipokea Neno la Mungu." Uombewe, naye Roho Mtakatifu alikuahidi uponyaji, basi sijali inachukua muda gani mpaka utakapokuja, bado tekeleza agizo lako, jifanye kana kwamba umeponywa, ukimsifu Mungu, endelea tu kusonga mbele. Hiyo ni kweli.

122 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, kamwe sijampokea Roho Mtakatifu bado." Kubali ahadi na uendelee kute-. . .Sasa, usiseme tu umempokea ati kwa sababu ulisema hivyo, hilo halitafanya kazi.

123 Vipi kama wanafunzi, baada ya wao kusema, "Yesu alitwambia twende huku juu sasa na kungojea, Yeye atatutumia ile Ahadi," na yapata siku tisa, labda Mathayo, ama baadhi yao huenda walikuja, ama tuseme, labda ilikuwa ni Filipo, ama baadhi yao, waliokuja na kusema, "Petro, hivi huamini tayari tumempokea? Hivi hufikirii tayari tumempata? Kwa sababu angalieni, Yeye alituagiza tuje huku na kungojea, mnaona, nasi tu—tumekuwa huku juu, hizi ni siku tisa. Mwajua, hivi majuzi kwa namna fulani nilijisikia, labda, kwamba tayari alikuwa ametupa Huo. Ninaamini afadhali tuukubali kwa imani na tuendelee"? Loo, jamani!

124 La, bwana, walikaa pale na kungojea mpaka ushahidi ukaja. Amina. Walikuja pale na kukaa mpaka walipoona kitu ambacho wangeweza kushika na kusema, "*Hiki* Ndicho." Kwa nini? Walikuwa na ushahidi wake wa Kimaandiko.

125 Walijuaje watampata? Isaya alisema katika Isaya 28:19, "Amri lazima iwe juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo, na huku kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo raha niliyosema wanapaswa kuona."

126 Yoeli, Yoeli 2:28 ilisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu; na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya wajakazi Wangu na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu." Walikuwa wakingojea jambo fulani litukie ambalo wangeweza kutazama na kuona. Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hebu tuone kile alichoahidi kufanya, hebu tukae nalo mpaka litakapokuja. Naam.

127 Nuhu alijenga safina moja kwa moja, akiishikilia, akihubiri wakati wote, akisimama moja kwa moja mlangoni mwa safina, akiwahubiria, akiijenga na kuwahubiria. Huyo ni nabii halisi wa Mungu siku hizi, akisimama moja kwa moja katika ile Safina, Kristo Yesu. "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu," endeleeni tu kujenga, mkiwashambulia popote walipo, mkiziba

kila shimo, msimwache ibilisi awe na kitanzi popote, la. La, bwana. Kaa moja kwa moja Mlangoni na kuhubiri, simama moja kwa moja Mlangoni mwa Safina na kuhubiri, Safina, Mlango, Kristo ndiye Mlango wa safina, hiyo ni kweli kabisa, "Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo." Na kwa hiyo kaeni papo hapo na kuhubiri.

128 Nuhu, kabla hajaona miujiza mikubwa ya Mungu kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, aliiona ile ahadi kwanza, akaipata ile ahadi, akaishikilia, na kuitekeleza ahadi hiyo mpaka akaona ule mwujiza mkuu wa Mungu. Amina. Naam. Ndipo akaona ule mwujiza mkuu wa Mungu.

129 Musa, akienda zake Misri akiwa na fimbo mkononi mwake, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, uvamizi wa mtu mmoja akishuka kwenda kuiteka akiwa na fimbo kuukuu, kavu mkononi mwake. Mnaona? A—alifanya hivyo pia. Hakika alifanya hivyo, hakika alifanya hivyo. Kwa nini? Alikuwa akitenda kazi. Unajuaje? "Vema, utakapofika kule chini, Farao atakunyonga. Amekuwa akikutafuta kwa miaka arobaini, na wakati wowote atakapokupata, hakika umekwisha. Ulimwua Mmisri, unajua mambo yalivyo, hata kumpiga Mmisri ni mauti, na hapa umemwua mmoja, na kumficha, na kukimbia. Utakaporudi kule chini, ni mauti." Lakini alikuwa akifanya nini? Akitenda kazi. Amina.

130 Sijui ilimchukua siku ngapi kufika kutoka huko chini Midiani, lakini alishuka. Loo, alishuka na ile fimbo mkononi mwake, kwa sababu alikuwa akitekeleza yale Mungu aliyomwahidi ya kwamba angefanya.

131 Sasa, kama Mungu akikupa ushahidi wa Roho Mtakatifu, kama alivyomtokea Musa katika Moto kule nyuma na kumfanya ajue ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, basi unapaswa, kama umemwona Mungu akiwaponya wengine, kama vile Musa alivyotupa fimbo yake chini wakati mmoja naye akajua angefanya hivyo tena, kuigeuza kuwa nyoka, alijua Yeye alikuwa Mungu na yale aliyofanya mara ya kwanza anaweza kuyafanya tena. Kama tu vile nabii alivyomwambia Gideoni, "Mungu wa baba zenu aliwapandisha kutoka Misri na kuleta miujiza hii yote na kadhalika, Yeye atafanya hivyo tena." Hiyo ni kweli.

132 Vema, Mungu aliyewaponya wagonjwa ndiye Mungu anayekuponya. Mungu aliyewapa Roho Mtakatifu huko nyuma ndiye Mungu anayekupa wewe Huyo. Mungu aliyemponya Hattie Waldrop *pale* kansa, akiwa amelala mauti mstarini, atakuponya. Hakika. Yeye ni Mungu, hivyo tu. Kama unatarajia kuona miujiza Yake mikuu pamoja na nguvu Zake, basi kwanza likubali Neno Lake na ulitekeleze. Hakika.

133 Musa alitenda kwanza, ndipo akaona miujiza mikuu ya Mungu. Wakati Mungu alipomwambia atembee kuelekea baharini, ilimbidi kuelekea baharini apate kuona hiyo miujiza

mikubwa. Chochote alichofanya, ilimbidi kumtii Mungu apate kuona miujiza mikuu ya Mungu; hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya.

134 Eliya, alipoenda huko juu ya mlima, aliwaita kule juu, kasema, "Hebu tuone ni nani atakayekuwa Mungu. Mungu anayejibu kwa Moto na awe Mungu," maana anajua ya kwamba Mungu ni Moto ulao. "Hebu Mungu aliye na Moto, ajibu."

Wakasema, "Hilo ni wazo zuri. Tutapanda kule juu."

135 Mbona, hakuogopa kwamba hao makafiri walikuwa na chochote. Walipoanza kumwita Baali na kujikatakata, na kufanya vituko, na kurukaruka juu ya madhabahu, alienda tu huku na huku, kasema, "Hebu mwiteni kwa sauti kubwa zaidi kidogo, labda anafuatilia. Labda anasinzia, ameenda kuvua samaki, ama chochote kile," mwajua, kuninii, kasema, "pigeni mayowe zaidi kidogo." Alijua mahali alipokuwa amesimama. Naam, bwana. Mtu ambaye amewahi kuwasiliana na Mungu na kupata agizo kutoka kwa Mungu, basi pepo wote kutoka kuzimu hawawezi kuutoa kwake, anajua mahali anaposimama. Bila shaka.

136 Akatembea huku na huko, ndipo alipofanya hivyo, akaweka chini dhabihu yake wakati wa kutoa sadaka ya jioni, akafingirisha yale mawe kumi na mawili kuonyesha ushirika, yale makabila yote kumi na mawili ya Israeli, kisha akaenda pale na kusema, "Sasa, Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli," akamwita jina Lake la kifalme, mnaona, "wa Israeli, na ijulikane, leo, ya kwamba Wewe ni Mungu, nami ni nabii Wako, nami nimefanya haya yote kwa Neno Lako."

137 Haya basi. Ilikuwa ni kitu gani? Kulitekeleza Neno Lake. Nini kilitukia? Moto ukashuka. Naam, bwana, uliiteketeza dhabihu. Aliona, na watu wote waliona, kazi kuu ya Mungu wakati alipotekeleza Neno la Mungu.

138 Yoshua, alizunguka ukuta huo sawa tu na jinsi Amiri Mkuu alivyomwambia afanye. Alikuwa nje alasiri moja akitembea, alikuwa akishangaa jinsi atakavyozivamia hizo kuta. Alijua ya kwamba alikuwa—alikuwa. . . adui alishindwa kwa sababu walikuwa ndani ya ukuta, lakini angeingiaje mle? Kwa hiyo akatembea kidogo alasiri moja apate kutafakari. Hilo ni jambo zuri, achana na kila mtu uwe peke yako kwa muda kidogo. Ndipo akamwona Mtu amesimama amechomoa Upanga wake, Yoshua alifikiri labda huyo labda, alikuwa ni mmoja wa hao wageni, kwa hiyo akauchomoa upanga wake, na kumkimbilia, akasema, "Je, wewe uko upande wetu, au wewe ni adui yetu?"

Akasema, "Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana." Naye akamwambia la kufanya.

139 Sasa, kwa namna fulani ni jambo gumu, kuwazia ungeweza kupiga tarumbeta na ukuta uanguke, lakini alichukua hatua. Mnaona, Mungu hulifanya rahisi sana na la kipumbavu, linapitia

moja kwa moja juu ya vichwa vya wenye elimu. Inahitaji hao wasio na elimu kuninii, ambao hawajui sana kulielewa, hivyo tu. Unapojaribu kuliwazia, huwezi kuliwazia, huna budi kuchukua Neno la Mungu kwa ajili yake, jinsi Yeye alivyosema lifanywe, si jinsi tunavyowazia kulifanya, bali jinsi Yeye alivyosema lifanywe. Jambo ndilo hilo, lifanye jinsi tu Yeye alivyosema lifanywe.

140 Basi Yoshua akasonga mbele sawasawa na ile amri. Basi nini kilitukia? Aliamini Neno la Mungu na kulitekeleza, ndipo akaona kuta zikianguka na adui akifa.

141 Wana wa Kiebrania, walikuwa wakitekeleza Neno la Mungu. Mungu aliwaambia hawapaswi kusujudia sanamu yoyote, wala hawapaswi kufanya hivyo. Kwa hiyo mfalme akasema, "Ama mtaisujudia, au nitawatupa katika tanuru ya moto."

142 Wakasema, "Sasa, ngoja kidogo, Mungu wetu anaweza kutukomboa, tunajua atakalofanya, bali hatutaisujudia sanamu yako, kwa vyovyote vile."

143 Kwa hiyo walikuwa wakitekeleza Neno la Mungu wakati Mungu alipofanya mwujiza mkuu, na kumtuma yule Mtu wa nne miongoni mwao, namna hiyo, na kuwakinga na moto. Walikuwa wakifanya nini? Wakilitekeleza Neno la Mungu ndipo wakauona mwujiza mkuu wa Mungu.

144 Tungeweza kusema mwingine, Danieli. Danieli alikuwa akitekeleza Neno la Mungu. Akainama kuelekea hekaluni, haidhuru ni nani aliyesema. Wao . . . Hakuionea haya dini yake, naye aliomba mara tatu kwa siku, akilitekeleza Neno la Mungu. Ndipo akaona jambo hilo.

145 Sasa, Gideoni, nitaharakisha, Gideoni, sasa, hakuwa na hakika, hakuwa na uhakika sana, huyu hapa Mzee ameketi, ameegemea kwenye mti, akimwambia la kufanya. Akasema, "Sasa, sijui. Nitafanyaje jambo hilo?" Akasema, "Ngoja hapa kidogo tu." Naye akaenda na kuchukua sadaka, akachukua sadaka, akaiweka juu ya madhabahu.

146 Maskini Jamaa huyu huenda alinyemelea pale na fimbo Yake namna *hii*, na kuigusa madhabahu hiyo, dhabihu ilitolewa, ndipo Gideoni alikuwa tayari kutenda kazi. Kwa nini? Alikuwa ameliona Neno la Mungu lililo hai likitenda kazi. Amina. Aliona Neno la Mungu lililo hai. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa akiishi katika hiyo—hiyo sanamu ya ukumbusho ya Mtu pale, ya kwamba Huyo alikuwa ni Mungu, alimwita, "Bwana."

147 Bila shaka, Yeye alitoweka. Akasema, "Malaika wa Bwana," ambalo ni dhihirisho tu, kama vile Yesu akiwa ni Mwana wa Mungu, hata hivyo Yeye alikuwa ni Mungu, Mungu alikuwa ndani Yake, bali hili ni dhihirisho, Malaika wa Mungu, kama aliyekuwa amekutana na Ibrahimu. Na hata hivyo Ibrahimu alimwita Mtu huyo B-w-a- . . . herufi kubwa, B-w-a-n-

a, "Elohimu." Mtu yeyote anajua, anayesoma Biblia ya Kiyunani, ama ya Kiebrania, anajua ya kwamba *Elohimu* ni Mwenyezi.

148 Mnaona, Yeye alikuwa pale katika huo, akidhihirishwa katika maskini—maskini mwili huo wa udongo uliowekwa pale. Jamaa mzee akiegemea kwenye mti kana kwamba amechoka, bali Yeye alichukua fimbo hiyo, na kuigusa dhabihu hiyo, nayo ikaunguzwa na Mwali wa Moto. Mnaona? Ndipo Gideoni akajua ya kwamba Hilo lilikuwa ni Neno lililo hai la Mungu, Gideoni alikuwa tayari kutenda kazi. Amina.

149 Ndipo baada ya kuwa tayari kutenda, Yeye alimpa elfu *kadhaa*, Yeye akasema, "Kuna waoga wengi sana humu ndani." Akaendelea tu, akaendelea, akawachonga, maana aliwapata waliokuwako, ambao Mungu alikuwa amewaita. Hiyo ni kweli. Wakati mwingine tunapoona mambo yakienda kombo, yakianguka, labda Mungu anatayarisha tu jeshi, hivyo tu, ama kuweka tayari baadhi ya wapiganaji, kamwe huwezi kujua. Mungu. . .Alikuwa tayari kutenda, alipoliona Neno lililo hai la Mungu, alikuwa tayari kulitekeleza. Tunapomwona Mungu akiishi katika Neno Lake, basi hebu na tuwe tayari kulitekeleza.

150 Kama tukimwona mwa—mwanamke ambaye ni duni sana hata mbwa wasingeweza kumtazama, halafu tumwone Roho Mtakatifu akimchukua mwanamke huyo na kumweka sawa na kumfanya mama, enyi wanaume, tunapaswa kuwa tayari kutekeleza Neno hilo lililo hai.

151 Usiku mmoja chumbani, natumaini sichukui wakati wenu mwingi sana, ni—niliingia chumbani wakati, uamsho mkubwa, nao walikuwa na chumba mara mbili ya ukubwa huu kilichojaa waliorukwa na akili, na wendawazimu, na kadhalika. Nikaingia humo chumbani, kulikuwako na mmoja wa wanawake warembo sana niliopata kuona ameketi pale, msichana, nikasema, "U hali gani?"

Naye akasema, "Njema, Ndugu Branham?"

Ndipo nikasema, "Vema, sijui nianzie wapi kwanza."

Akasema, "Labda nami."

152 Nikasema, "Ati nawe?" Mbona, alikuwa msichana mzuri, safi, macho makubwa ya hudhurungi, na mrembo, na nywele ndefu zikining'inia mgongoni mwake, na—naye alikuwa ni mwanamke mwenye sura nzuri sana. Nami nikasema, "Wewe si mgonjwa."

Akasema, "Naam, ni mgonjwa."

Nikasema, "Katika mahali hapa pa wendawazimu?"

Akasema, "Naam, Bwana."

Nikasema, "Kwani ilikuwaje?"

Naye akasema, "Vema, ningetaka usikie hadithi yangu."

Nikasema, "Endelea moja kwa moja, Dada, ningetaka kusikia."

153 Akasema, "Vema, Ndugu Branham," kasema, "nilipokuwa msichana," kasema, "nililelewa na wazazi Wakristo ambao kweli walimwamini Mungu." Kisha akasema, "Nilienda kanisani." Lakini kasema, "Mara nikaanza kuambatana na mvulana aliyevuta sigara," kisha kasema, "Ilitokea kwamba niligundua kwamba alikunywa pombe. Ndipo usiku mmoja alitaka kunifanya ninywe pombe, wala nisingefanya hivyo," kasema, "Kabisa nisingefanya hivyo. Ndipo akanishawishi kula peremende," ama, la, ilikuwa ni "kunywa Coke," "usiku mmoja, naye alikuwa ametia kitu fulani ndani yake." Kisha kasema, "Sikuwa msichana mwadilifu tena." Halafu kasema, "Ndipo nikawazia, 'Kuna faida gani?'" Kasema, "Nikayatupilia mbali tu maisha yangu, nami nikawa kahaba wa kawaida wa mitaani." Kisha kasema, "Ndipo ni—ni—nikafanya tu kila kitu kilichokuwa kibaya, nikaanza kunywa pombe, nikawa mlevi sugu."

154 Naye akasema, "Ndipo mtu fulani akaniambia nibadili dini yangu, nikaondoka nikaenda kwenye Nyumba ya Mchungaji Mwema katika kanisa Katoliki, nikabadilisha dini yangu. Wakanipeleka kule juu kwa miaka miwili ama mitatu," kasema, "nilifanya vizuri, nikarudi huko nje." Kasema, "Niliporudi huku nje, nikaruidia moja kwa moja tena." Tena akasema, "Niliendelea hivyo kwa yapata mwaka mmoja, sheria ikanikamata na kunipeleka kwenye gereza la wanawake, nami nikafungwa huko miaka miwili," kisha kasema basi, "kwa ajili ya uhalifu."

155 Kisha—kisha kasema, "Ndipo mimi, halafu baada ya kutoka mle, nikarudi," ndipo kasema, "Na—nakwambia, Ndugu Branham," kasema, "hiyo imekuwa tu yapata miezi miwili ama mitatu iliyopita," kasema, "Nimerudi nikifanya jambo lile lile nililofanya sikuzote."

156 Nami nikasema, "Vema, hiyo ni aibu." Nikasema, "Mwanamke mrembo kama wewe, hivi huwazii juu ya kupata mume wakati fulani, na watoto wachanga, na kama vile mwanamke yeyote angefanya, aliye na sifa yoyote ya *kike* ndani yake?"

157 Akasema, "Loo, naam, Ndugu Branham." Akasema, "Ni nani angenitaka mimi?" Mnaona? Kasema, "Ningeweza kumpa nini mwanamume?" Kasema, "Mimi, si kitu ila maisha katili, ninalewa na kupiga mayowe na kadhalika." Kasema, "Ningefanya nini?"

Nami nikasema, "Vema, Mungu anaweza kunyosha hilo."

Akasema, "Bw. Branham, nimeomba na kufungua kurasa mpya na chochote kile," kasema, "Kamwe si—si—sijui nina shida gani."

158 Nikaendelea, nikiishika tu roho yake kuona kuna shida gani, mnaona. Nami nikaendelea tu kuangalia kwa dakika chache, ndipo akasema . . . Nikasema, “Vema, sasa, nitakwambia, labda mimi na wewe tutaomba.”

Akasema, “Vema, Ndugu Branham.” Akashuka nasi tukaomba.

Kisha nikasema, “Hebu omba sasa.”

Naye akaomba, akasema, “Mungu,” naye akaomba na kuomba. Baada ya kitambo kidogo akasimama na kuniangalia, akasema, “Vema, Ndugu Branham . . . ”

Basi nikaweka mkono wangu begani mwake, na kusema, “Mungu akubariki, Dada.”

Naye akasimama, akasema, “Ninaamini yote yamekwisha sasa.” Akasema, “Nitaondoka hapa na kujaribu kuishi maisha tofauti.”

159 Nikasema, “Dada, utatoka uende ukaishi maisha yale yale uliyoishi,” Unaona? Nikasema, “Unafungua ukurasa mmoja tu,” nikasema, “bado si sawa.” Kwa hiyo nikasema, “Hebu na tuombe zaidi.”

160 Ndipo tukashuka, tukaendelea kuomba, baada ya kitambo kidogo akagonga Kitu fulani. Jamani, ilibadilika, naam, bwana, kutoka kama mtoto mdogo akibonyeza-bonyeza *muziki* mpaka akaanza kucheza muziki, naam, bwana, ina mdundo fulani ndani yake, mwajua. Baada ya kitambo kidogo akaanza kuomba kwelikweli, na baada ya kitambo kidogo akaanza kupiga mayowe, huku machozi yakitiririka kwenye mashavu yaliyopakwa rangi, juu, namna hiyo, moja kwa moja, alipoyainua hayo macho makubwa mno ya hudhurungi, akaniangalia, alisema, “Ndugu Branham, jambo fulani limetukia.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

161 Naam, bwana. Ameolewa na ana watoto watatu ama wanne sasa. Ilikuwa ni kitu gani? Alimchukua Mungu na kukaa nalo mpaka jambo fulani likatukia. Jambo ndilo hilo. Jambo fulani lilitukia, Neno lililo hai likawa uhalisi ulio hai kwake.

162 Basi Mungu anapoweka ahadi Yake ndani yako na inakuwa uhalisi ulio hai, basi kitu fulani ni tofauti. Kamwe huendi tu na kusema, “Naam, ninaamini,” sasa, hiyo ni sawa, ibilisi analiamini hivyo, bali limethibitishwa kwako, ndipo ma-. . . Neno linakuwa hai ndani yako, ndipo unaanza kuona ni Kitu gani. Naam.

163 Yohana Mbatizaji, alikuwa . . . Ni ajabu, baba ya Yohana alikuwa ni kuhani, tunajua hilo, ya kwamba alikuwa ni kuhani, na badala ya kutoka sasa wakati wewe . . . Nadhani kidogo ilikuwa ni vigumu kwake na mama yake ku—kumpata huyo mtoto Yohana, akiahidiwa jinsi alivyokuwa, naye alikuwa

anaenda kuwa mtu mwenye nguvu wa Mungu, bali walijua kamwe hawangeishi kuona jambo hilo, maana walikuwa wanazeeka sana. Basi yapata umri wa miaka tisa wanasema baba na mama yake walikufa.

164 Ndipo badala ya Yohana kurudi kwenye, kusomea ukuhani, alijua, Yohana alijua, alikuwa amtangaze Masihi, kwa hiyo badala ya kushuka kwenda kusoma shuleni, na kupata Shahada ya Kwanza ya Sanaa na Ph.D., na LL.D., na Q.U.S.T, na hizo zingine zote, mwajua, zinazoambatana nazo, kwa hiyo basi, badala ya kwenda kuchukua hayo yote, aliondoka akaenda nyikani, maana Ujumbe hauna budi kutoka kwa Mungu. Naye Mungu. . .

165 Sasa, alijua kungekuwako na ishara za kila namna, na kila namna ya *hii*, maana ndivyo ilivyo sikuzote, udanganyifu na kadhalika, maana inafanya tu hivyo ipate kuficha kitu halisi. Kuna watu wengi sana wanaotenda kana kwamba wana Roho Mtakatifu, nao wanatoka nje na kuishi maisha ya namna yoyote ile, hao ni maskini vitisha ndege, kujaribu kukuogopesha uachane na kitu kilicho halisi.

166 Vitisha ndege vyote viko wapi? Sio juu ya mtofaa uliochachuka, kwenye mtofaa mzuri, hiyo ni kweli, ndipo palipo na vitisha ndege. Naye ibilisi huweka kila namna ya vitishio kuzunguka kitu halisi, hapaswi kuwa na wasiwasi kuhusu huo mwingine, hawatasumbua kwa vyovyote vile. Kwa hiyo basi, wao. . . Unapokuwa na kitu hicho halisi, hapo ndipo vitishio huinuka, hapo ndipo dola ya bandia imekaribia sana, mwajua, kuwapoteza walio Wateule kama yamkini, alisema Yesu, mnaona. Hapo ndipo unapoangalia, moja kwa moja kwenye mstari huo hapo, unaona.

167 Kwa hiyo basi tunaona ya kwamba Yohana hakutaka kuchanganyikiwa kabisa, kwa hiyo alingojea huko nje mpaka aliposikia kutoka kwa Mungu, ndipo Mungu akamwambia ni ishara ya namna gani ambayo Masihi angekuwa nayo. Kwa hiyo Yohana alikuwa akitekeleza Neno la Mungu. Walishuka wakaja na kusema, "Yohana, wewe ni Masihi?"

Kasema, "La."

Kasema, "Wewe ndiwe *yule* Nabii?"

Kasema, "La."

"Wewe ni Yeremia, Isaya, Eliya, mmojawapo?"

168 "La." Kasema, "Mimi siye, bali Yeye anasimama katikati yenu mahali fulani sasa. Kuna Mtu miongoni mwenu sasa." Alikuwaje na hakika hivyo? Kwa sababu alijua wakati ulikuwa umewadia kwa Neno la Mungu kutimia. Amina.

169 Kile tunachopaswa kufanya leo, ndugu. . . Wakati umewadia wa Neno la Mungu kutimia. Wakati umewadia ambapo ishara zinamfuata mwaminio. Ni wakati wa Nuru za jioni kuanza

kuangaza. Ni wakati wa Yesu Kristo kujidhihirisha Mwenyewe yeye yule jana, leo, na hata milele.

170 Hili si fundisho, huu ni msemo, kumbukeni, hebu nilinukuu tena, si fundisho, msemo, kufanya mfano: Mungu aliandika Biblia tatu, moja ya Hizo ilikuwa angani, mwanadamu kuangalia juu apate kutambua Muumba wake ametoka huko, zodiaka. Kitu cha kwanza ni kipi katika zodiaka? Inaanza na bikira. Umbo la mwisho katika zodiaka ni nini? Leo, yule simba.

171 Mara ya kwanza Kristo alipokuja ilikuwa ni kupitia kwa bikira, wakati mwingine atakapokuja ni kupitia kwa Simba wa kabila la Yuda. Wale samaki waliokingamana, ule wakati wa kaa, na kadhalika, mlivyoyasoma yote, kama Ayubu alivyoyachunguza, nanyi mnaosoma Kitabu cha Ayubu, mtaelewa. Sasa, ibilisi, bila shaka, huchukua na kufanya mambo kwa hiyo.

172 Kisha tunarudi kwenye lingine wanaloliita fundisho la piramidi. Kamwe msiyafuatilie, mnayo Biblia ya kufuatilia. Mnaona? Sasa, iliyofuata ilikuwa ni ile piramidi, lakini laiti ungalipata maana halisi nyuma yake! Sasa, angalia ile piramidi kwa ajili ya wakati wa kanisa. Hivi ulijua . . . ? Angalia . . . Je, una noti ya dola? Angalia upande wake wa nyuma. Kuna piramidi, upande wa pili, kuna muhuri wa Marekani. Kwa nini Marekani itambue chini ya piramidi, "Ule Muhuri Mkuu"? Angalia tu juu ya lile jiwe la kuwekwa juu, lililowekwa juu ya hiyo piramidi, nawe utaliona limesimama huku nuru ikiangaza pande zote. Unaona? Liko huko juu kwa kusudi gani? Huo ndio ule Muhuri Mkuu.

173 Kwa nini hilo halikuninii . . . ? Kamwe hawakuweka kifuniko juu ya hilo jiwe. Nimekuwa kule kwenye piramidi. Kwa nini hawakuweka kifuniko juu yake? Kwa sababu kilikataliwa. Hilo lilikuwa ndilo jiwe kuu la pembeni, ambapo mawe mengine yote yaliunganishiwa, lilikuwa likizungumza juu ya wakati wa kanisa.

174 Angalia huku chini kabisa kwenye wakati wa Kilutheri, huko nyuma kabisa katika walio wengi, huko nyuma, kukiri tu kwamba Kristo alikuwa wangu, kunamaanisha tu kuwa Mkristo, kuhesabiwa haki. Moja kwa moja akaja Wesley, utakaso, nyembamba kidogo, utakaso. Ndipo ikaja Pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ni kitu gani? Kuumbika, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

175 Sasa, Yeye anafanya nini? Hilo halina budi kuchongwa kikamilifu sana, Kanisa hilo liletwe mahali hivi kwamba, hata lile Jiwe linalokuja litoshee juu Yake . . . Mnaona ninalomaanisha? Hilo hulitengeneza Kanisa. Na kupitia hayo yote ni Kanisa. Sasa, hiyo—hiyo ni ninii tu, hiyo ni kufanya mfa—mfano ninaozungumzia, usijaribu kuingia ndani yake.

176 Halafu, Biblia inayofuata, Biblia halisi, ni *Hii*. *Hii* ni Neno letu. Ishara tu na kadhalika walizokuwa nazo huko nyuma . . .

177 Lakini angalieni, jinsi jiwe hilo lilivyo kamilifu, lilikataliwa, kamwe hawakuliweka juu yake. Kwa nini? Na kama ukienda kule, hayo mawe juu kwenye piramidi hiyo yenye uzito wa maelfu ya tani, ambayo yameshikamanishwa sana hata huwezi kuupenyeza wembe, na hakuna saruji ndani yake, yamechongoka kikamilifu. Basi kama ilibidi hayo kuwa hivyo kufanya kila wakati ushikane pamoja, basi itakuwaje wakati kule kuja . . .?

178 Hivi hamlioni Kanisa likiumbika? Luther, kuhesabiwa haki; Wesley, utakaso; ndipo akaja Roho Mtakatifu. Na sasa, Kanisa likichongwa na kutengenezwa basi, bila waa wala kunyanzi, kusudi Yeye asiyekuwa na doa wala kunyanzi aweze kushuka na kuliunganisha pamoja kwa ajili ya ufufuo, kusudi Kanisa la Mungu aliye hai liruke liingie kwenye . . . Naam. Mnaona? Naam. Sasa, tunaishi katika siku hiyo.

179 Sasa, Yohana alikuwa akitazamia hilo kuja, akasema, "Nitamjua, Yeye yuko huko nje, sijui alipo. Amesimama huko nje."

Labda askofu fulani alikuja na kusema, "Unajua, nimekuwa na hisia ya kipekee ikinipitia kwa muda, mwajua, labda mimi ndiye Masihi."

Akasema, "Ondoka." Kasema Yohana, "Huyo siye." Vema.

180 Huyu hapa mwingine anakuja, kasema, "Vema, unajua nini? Nina digrii ya juu kuliko zote, mimi ni Kayafa, kuhani mkuu, kama kungekuwa na mtu yeyote aliyetiwa mafuta awe Masihi, mwanadamu, ingekuwa ni mimi."

181 "La, la, la. La, huyo si Yeye." Lakini Yohana alisema, "Yeye aliyeniambia kule nyikani niende nikabatize kwa maji alisema Ambaye nitamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

182 Pia kumbukeni, Yohana aliiona wala hakuna mtu mwingine aliyeiona. Ilikuwa ni ishara aliyopewa Yohana kuiona hiyo, naye aliiona, na Yohana alikuwa na hakika, na sababu ya yeye kuweza kutangaza, "Huyo ndiye Masihi!"

"Unawezaje kuwa na hakika?"

"Ninafuata Neno la Mungu."

183 Ninawezaje kuwa na hakika mtu huyu ni mwaminio? Ninafuata Neno la Mungu, Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Si kwa sababu ana Digrii ya Sanaa, kwa sababu yeye ni Ph.D., ama LL.D., ama askofu, kasisi, kadinali, ama papa. Mnaona? Hilo halina uhusiano wowote nalo, hayo ni mapokeo ya kujibunia. Haleluya!

184 Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa Jina Langu watatoa pepo," basi hata wanalikana, mnaona, "watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya." Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

185 Alifanya kazi za aina gani? Haya basi. Je, aliandaa shule? Akawatuma wanafunzi Wake kwenda shuleni? Je, alimfundisha Petro elimu? Hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Biblia ilisema yeye na Yohana hawakuwa tu wasio elimu bali walikuwa wasio na maarifa.

186 Wasio na maarifa wala elimu, bali walikuwa na kitu cha kumpa huyo mtu, fedha na dhahabu, hazikuwavutia, hawakuwa na elimu, "Lakini nilicho nacho, nitakupa: Katika Jina la Yesu Kristo simama uende." Haleluya! Huo ulikuwa ndio utambulisho wao. Hilo ndilo walilohitaji. Walikuwa wakifuata Neno la Mungu, ndipo wakaona mwujiza wa Mungu, walipolifuata Neno la Mungu.

187 Paulo, akiketi, akihubiri wakati mmoja, alikuwa amemwona mtu aliyekuwa na imani, kasema, "Naona una imani ya kuponywa. Simama." Haya basi. Naam, bwana. Ilikuwa... Alikuwa ni kitu gani? Unataka kuona mwujiza wa Mungu? Lifuate Neno la Mungu.

188 Upesi, Martha, loo, jamani, maskini mtu huyo alikuwa amevunjika moyo, alikuwa ameacha kanisa lake kubwa, yeye na Mariamu, walikuwa wamemkaribisha Yesu, wakamtengenezea mahali padogo huko Bethania, baada ya Yeye kuwa, hakuwa na mahali pa kuishi, wakampa makazi kule pamoja nao, pamoja naye, na Martha, na Mariamu, na Lazaro. Nao walidhani ya kwamba Yeye hakika alikuwa ndiye Masihi, na yote haya. Ndipo ndugu yake akawa mgonjwa.

189 Mnaona jinsi Mungu anavyoachilia mambo yatendeke? Anawararua tu nyote vipande-vipande ili kuwajaribu. Kila mtoto amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa na kupim-... "Msione kuwa ni ajabu, wapenzi, majaribu makali yanapokuja, yote yanafanywa ili kuthibitisha imani yenu." Mnaona?

190 Na kwa hiyo Yesu akaondoka, Naye akasema anaondoka. Na kwa hiyo basi wakaagizia aitwe, kasema Lazaro alikuwa mgonjwa, kwa hiyo wakatuma mtu, kasema, "Yule umpendaye ni mgonjwa." Yesu hakulijali hata kidogo, akaendelea moja kwa moja, akaenda kwenye mji mwingine, ndipo wakimbiaji zaidi wakaja na kusema, "Lazaro ni mgonjwa, karibu kufa, rudi." Yesu akapuuza tu kana kwamba hakuna kitu kilichotukia, akaendelea moja kwa moja.

191 Mnaona, tayari alikuwa ameona yale Baba aliyokuwa anaenda kufanya, maana Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno

mpaka amwone Baba akilitenda. Na yale Baba anayomwonyesha Mwana, hayo ndiyo Yeye. . .Mimi natenda-. . .Yeye anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa." Mnaona? "Mimi hufanya tu yale anayonionyesha nifanye."

192 Sasa, Yeye hakusema uongo, hawezi kusema uongo, hakufanya mwujiza hata mmoja mpaka kwanza Mungu alipomwonyesha, kwa ono, jambo la kufanya, Yohana Mtakatifu 5:19. Kama sivyo, Neno hilo si sahihi, basi kama si sahihi, tunasoma Biblia ya namna gani? Mnaona? Yote imevuviwa, vema, mnaona, lakini Yeye alifanya hivyo, na manabii wote, kama tu vile Mungu alivyowaonyesha la kufanya.

193 Alipita pale na kumponya mtu huyo aliyekuwa amelala pale aliyekuwa na ugonjwa wa tezi dume, ama TB, ama *kitu fulani*, alikuwa nao miaka thelathini na minane, ulikuwa umedumaa, haukuwa unaenda kumwua. Akawaacha maelfu wamelala pale viwete, vipofu, vilema, na waliopooza, akawaondokea moja kwa moja kwa sababu hivyo ndivyo. . .Alisema alijua ya kwamba mtu huyo alikuwa katika hali hiyo kwa muda huo. Mnaona? Ndipo akawaambia, "Siwezi kufanya lolote mpaka Baba anionyeshe la kufanya."

194 Sasa, tunaona, bila shaka hiyo ilikuwa ni dosari kubwa, waliwazia, hilo, dhidi Yake, bali Yeye alitenda tu ili kumpendeza Mungu. Na mtu yeyote anayemtumikia Mungu atatenda kumpendeza Mungu, atafanya yale Mungu anayomwambia afanye, kabisa.

195 Martha, alijua kwamba Yeye alikuwa hivyo. Baada ya kitambo kidogo. . .Sasa, Martha, walikuwa wakisema ya kwamba yeye hakuwa, alikuwa mzembe na kadhalika kuhusu kuisafisha nyumba yake, lakini wakati shindano la kuamua lilipokuja, alionyesha rangi yake. Naam, bwana. Mariamu alikuwa ameketi akilia, kwa sababu ndugu yake alikuwa amekufa, lakini Martha alitoka akaenda akakutana na Neno lililo hai. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

196 Yeye alikuwa ni Neno lililo Hai la Mungu, hiyo ni kweli, Neno la Mungu lililodhihirishwa. Si ajabu Yeye angeweza kusimama na kutambua mawazo ya watu. Sasa, Biblia ilisema. . . Ulisema, "Loo, hilo ni Neno?"

197 Naam, bwana. Naam, bwana. Hivi huijui Biblia? Waebrania 4 ilisema, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo," Neno la Mungu, wakati likiwa ndani yako. Naam, bwana, unaona. Neno la Mungu likidhihirishwa ndani Yake.

198 Kwa hiyo Martha, wakati alipokuja na kuanguka miguuni Pake, naye akasema, "Bwana," *Bwana*, hivyo ndivyo

Yeye alivyokuwa, “kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Akasema, “Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.” Loo, haya basi, haya basi, “Haidhuru umefanya nini, msimamo Wako, Wewe unafuata yale Mungu aliyosema ufanye, kama Wewe ulisema *hivi* ama *vile*, ama kama Wewe ulikuja, ama hukuja, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

Kasema, “Ndugu yako atafufuka tena.”

Kasema, “Naam, Bwana, atafufuka katika siku za mwisho. Atafufuka, alikuwa mtu mwema, ata—atafufuka katika ufufuo wa kiama.”

199 Akasema, “MIMI NDIMI Ufufuo na Uzima, yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Hakuna mtu angaliweza kusema hivyo ila Yeye. “Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?”

Akasema, “Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, aliyekuwa aje ulimwenguni.” Haya basi.

200 Ni kitu gani? Anatenda kazi. Anataka kuona mwujiza, kwa hiyo anatafuta kujua kile Neno lisemacho. “Ninaamini Neno, limesimama hapo katika umbo la Mwana wa Mungu. Maneno Yake si Yake, ‘Si Mimi ninenaye, bali ni Baba akaaye ndani Yangu.’ Lolote litokalo kwenye maskini midomo Yako inayonena, nitaamini ni agizo la Mungu.” Loo, ndugu! Hmm! “Wewe ndiwe Masihi.” Masihi ni nini? Aliyetiwa mafuta. Mnaona? “Wewe ni Mtiwa mafuta wa Mungu.”

201 Mungu alikuwa na mtiwa mafuta kwa kiwango kidogo siku moja, na jina lake lilikuwa Eliya, Basi kulikuwako na, ama, Elisha, naye mwanamke mmoja alikuwa na mtoto mchanga naye akafa, ndipo akamwendea mtumishi huyu wa Mungu, naye akasema, “Ewe mtu wa Mungu,” alimtambua, basi huyo mtiwa mafuta wa Mungu akaja na kutembea kote sakafuni, loo, jamani, akaulaza mwili wake juu ya maskini mtoto huyo aliyekufa, naye akapiga chafya mara saba kisha akafufuka.

202 Na kama Mungu alifanya hivyo kwa nabii Wake aliyetiwa mafuta, ni zaidi sana vipi atafanya kwa Imanueli? “Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu.” Kama kamwe utapata chochote kutoka kwa Mungu, huna budi kumwamini mtumishi wa Mungu, Neno la Mungu. Unaona? Naye alikuwa ni Neno. “Ninaamini, niambie tu la kufanya.”

203 “Mmemweka wapi?” Akashuka akaenda kaburini, akilia kama mwanadamu. Alipofika kule chini, Yeye alisema sasa ufanye nini utakapofika hapa? Mnaona, wana jambo la kufanya pia, mwajua. Kasema, “Liondoeni hilo jiwe, mkitaka kuona mwujiza.”

204 Ninyi watu wagonjwa usiku wa leo, kama mkitaka kuona mwujiza, liondoeni jiwe. Liondoe jiwe hilo, dhambi hiyo iliyo

mlangoni. Ni kitu gani? Unasema, “Ndugu Branham, sifanyi chochote.” Lakini kama huliamini, haliwezi kutukia. Liondoe hilo jiwe la kutokuamini uone kitakachotukia, liondoe tu hilo jiwe. Basi alipotii Neno la Bwana, aliona mwujiza. Hakika.

205 Yule mwanamke kisimani, kwa namna fulani alikuwa chini ya. . .hakujua la kusema. Alimwona Myahudi huyu ameketi pale, “Sasa, ni ajabu kwamba Myahudi huyo angezungumza nami, mimi ni mwanamke Msamaria. Sijui sababu Yake ni nini?” Akasema, “Vema, mnasema, ninyi Wayahudi husema, ‘Abuduni Yerusalemu,’ baba zetu waliabudu katika mlima huu.”

206 Akasema, “Mwanamke, nakwambia sasa, ya kwamba si Yerusalemu, wala katika mlima huu, bali Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.”

207 Alijua hilo lilisikika sawa. Kama Mungu ni Mungu wa mmoja, Yeye ni Mungu wa wote, viumbe Vyake vyote. Naam, bwana. Kwa hiyo alionekana. . .Mwajua, jamii yake na kabila na rangi hawakuwa na uhusiano wowote, Mungu aliwaumba wote, “Mungu kwa mtu mmoja alifanya mataifa yote kutoka kwa Adamu.” Hapo tunaona ya kwamba rangi ya ngozi na ninii, mapokeo yao, ama ushirika wao wa kanisa havikuwa na uhusiano wowote nalo, Yeye anatafuta moyo mwaminifu.

208 Kwa hiyo akaangalia chini pale. . .Naye akaona tena, akasema. . .Na halafu muda si muda mwajua, wakati alipowasiliana naye na kujua mahali shida yake ilikuwa, amekuwa akiishi na mwanamume mwingine, Naye akasema, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

Akasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

209 Akageuka. Ati nini? Alikuwa amekutana na Neno lililo Hai. Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sasa, hatujui kuhusu kuinuka kwa nabii yeyote katika siku hii, bali tunajua ya kwamba Masihi ajapo, hiyo itakuwa ndiyo ishara ambayo Yeye atatuonyesha. Yeye atatuambia mambo haya.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Loo, jamani!

210 Aliona nini? Mji mzima ukamgeukia Mungu. Kwa nini? Alilifuata Neno la Bwana. “Mimi ninayenena Ndiye.”

211 Ndipo akakimbia mjini na kusema, “Hebu na tusome Maandiko. Hivi Biblia haisemi hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi? Njoni, mwone Mtu hapa nje aliyeniambia mambo yale yale ninayofanya.”

212 Unajuaje? Kama tu vile Yohana alivyofanya. Unajuaje Yeye amesimama miongoni mwenu? Ni wakati wake. Unajuaje ndivyo ilivyo? Huyo ndiye Masihi Mwenyewe, kwa sababu wakati wa Masihi wa kutokea umewadia.

213 Hivi hamwoni ninalomaanisha? Wakati umewadia kwa Kanisa hili kusimama kwa miguu Yake. Ni wakati wa kundi la Kipentekoste kuamka. Jiondoe kwenye mapokeo yenu ambayo unajitikisa kuingia ndani yake. Jitikise, na ujiulizie njia ya kale. Kwangua mavumbi ya kikanisa yakuondokee, simama katika Jina la Yesu Kristo. Simama, na umkubali Mungu kwenye Neno Lake na usonge mbele.

214 Kama Mungu yu pamoja nasi, iko wapi miujiza Yake? Iko wapi? Tunaona wapi ishara hizo? Ikiwa Mungu yuko katika makanisa haya yote na minara hii mikubwa ya kikanisa, na kadhalika, na Ph.D. hizi zote na kadhalika, nionyeshe miujiza Yake. Mungu yuko wapi? Utukufu! Hiyo ni kweli. Yuko wapi Mungu? Iko wapi miujiza Yake? Mahali Mungu anapotokea, Yeye ni wa kimbinguni, ishara Zake za kimbinguni hufuatana na Mungu wa kimbinguni. Mungu ni . . . Iko wapi miujiza Yake yote?

215 Aliona mwujiza wa Mungu, ishara ya Masihi. Alisababisha mji mzima, Biblia ilisema ya kwamba watu wote, Yesu hakufanya hivyo tena, waliamini ushuhuda wa huyo mwanamke. Alikuwa na majaliwa basi ya kuuongoza mji wote kwa Kristo, kwa sababu alifuata Neno Lake na ninii Lake, na kuona kwamba Yeye angeweza kufanya mwujiza, alijua ya kwamba ndivyo ilivyokuwa.

216 Wapentekoste, Wapentekoste mia moja na ishirini, walioondoka, baada ya kumwamini Yeye, walienda na kumtii, wakangojea katika chumba cha juu mpaka walipopewa Nguvu zitokazo Juu. Waoga, walishusha mapazia ya dirisha, wakafunga madirisha, maskini chumba kidogo cha juu, wakatoka nje ya hekalu, wakapita kando na kuingia kwenye mlango, huko juu kwa siku kumi mchana na usiku, wakingojea tu.

217 Ndugu, wakati Neno lilipodhihirishwa, walitoka madirishani na milangoni na kuingia mtaani, jambo fulani lilikuwa limetukia. Kwa nini? Walikuwa wameona mwujiza, waliona Nuru, kama ndimi za Moto, zimemkalia kila mmoja wao. Walihisi nguvu za Roho Mtakatifu zikitikisa. Waliona na kuhisi pia, walijua jambo fulani lilitukia. Wakakimbia nje kujaribu kushuhudia jambo hilo na hata wasingeweza kuzungumza lugha yao wenyewe. Jambo fulani lilitukia.

218 Tatu ni ushahidi. Waliihisi, wakaiona, nao wakaiangalia ikijidhihirisha, wakaihisi, wakaiona, na kuisikia. Amina. Tatu ni ushahidi. Naye huyo hapo, hata hivyo, waliiona. Vivyo hivyo sasa, ahadi Zake zote, ukitaka kuziona zikidhihirishwa, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kulitimiza tu Neno Lake. Litii Neno Lake Naye atalifanya. Loo, jamani. Vema.

219 Kama ukitoka hapa nje siku yoyote, kama wakati ni moja kwa moja mchana . . . Unaamini wakati wa Masihi kutokea umewadia? Unaamini wakati umewadia kwa Kanisa kuonyesha Uwepo Wake, kuonyesha Uwepo wa Kristo? Na badala tu ya . . .

unataka kwenda kanisani na kujiunga na kanisa na kusema, “Sisi Wapresbiteri,” “Sisi Wabaptisti,” “Sisi Wamethodisti,” “Sisi Wapentekoste,” “Sisi *Hiki-na-hiki*,” na “Sisi, sisi—sisi—sisi ndio, tu—tuna *hiki* na tuna *kile*.” Siku hiyo imekufa kama usiku wa manane, hiyo ni kweli, mnaona, kufanya hivyo tu. Hiyo ni kweli. Lakini ni wakati wa Nuru za jioni kuangaza, kama vile wimbo unavyosema, “Itakuwa nuru wakati wa jioni.” Ni wakati wa Nuru hizo za jioni kuangaza, huu ndio wakati.

220 Sasa, ni kitu gani cha kulizuia kuangaza? Hebu toka nje siku yoyote, siku yoyote utakayo, kisha urudishe tu mawingu yote nyuma, nalo jua linawaka haidhuru. Jua linawaka wakati wote, yasogeze tu hayo mawingu. Mungu yeye yule aliyeponya, Mungu yeye yule aliyejaza na Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule, aliyetimiza kila ahadi, ni, M-w-a-n-a wa Mungu anaangaza wakati wote, ondoa tu hayo mawingu ya mashaka. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

221 Lakini tuna mawingu mengi ya kikanisa ambayo yamemtia uvuli mbali nasi. Madhehebu mengi na upuuzi umemficha Kristo kutoka kwetu. Yarudishe tu nyuma, kwa maombi, kila moja ya hayo mawingu ya kale uone kama Kristo haonekani kama alivyowahi kuwa, kama Yeye hataonekana katika Nuru ile ile, nguvu zile zile, ishara zile zile, ajabu ile ile, uone kama Yeye si Masihi yule yule bado. Amina. Yarushe mawingu yote, ukiyapeperusha yarudi kutoka upande mmoja, uone kama sivyo. Hakika. Kama wewe. . .Lakini jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kuamini na kutenda. Sasa, hiyo ni, ninii, kweli.

222 Yule shujaa alikuwa sahihi, “Kama Mungu yu pamoja nasi, basi hebu tuone miujiza Yake.” Iko wapi miujiza yote? Ziko wapi ishara? Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele, basi iko wapi ishara kwamba Yeye ni yeye yule? Aliahidi nini? Yohana Mtakatifu 14:12, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Iko wapi? Aliahidi jambo hilo, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” wakati Mungu aliposhuka. Hatujui kamwe Mwili huo ulienda wapi.

223 Kulikuwa na wale watatu, Malaika watatu. Mmoja Wao alikuwa ni Mungu Mwenyewe aliyeshuka katika umbo la mwanadamu, akasimama pale na kula pamoja na Ibrahimu. Hiyo ni kweli. Alisimama pale na kuzungumza na Ibrahimu kuhusu ha-. . .yale mambo, akasema, “Sitamficha jambo hili Ibrahimu. Ninashuka kwenda Sodoma, nilisikia kwamba ni waovu mno, ninashuka kwenda kutafuta kujua.” Ibrahimu alimlisha maziwa, ugali, keki za mahindi, mwajua, ugali, na vipande vya nyama ya ndama, Naye akala. Kweli.

224 Unasema, “ati Mungu akala hicho?” Yesu alikula baada ya kufufuka Kwake. Hakika, alikula. Hakika. Alisimama pale na kula. Baadhi yao walisema, “Huyo hakuwa Mungu.” Vema basi,

Ibrahimu alikosea basi, alimwita, "Elohimu." Alimwita, alikuwa ni Mungu.

225 Mungu, Yeye alikuwa akifanya nini? Alikuwa akionyesha jambo fulani. Kama tu vile alivyomfukuza mjakazi na mtoto wake, kwamba nanii, mwanamke huru na mtoto wake, hiyo ndiyo sababu Ibrahimu hakutaka kumwoa Hajiri. Lakini Yeye...mke...Yeye akasema, "Mwoe. Sikiliza yale Sara akuambiayo," kwa sababu ilibidi yatimizwe.

226 Ilimbidi nabii kulala kwa ubavu wake kwa muda wa siku mia *kadhaa*, kisha upande huo mwingine. Nini? Kwa ajili ya ishara. Naye alikuwa akionyesha ishara pale. Mungu akidhihirishwa katika mwili, kasema, Yesu aligeuka, Mwanawe, alipokuja duniani na kusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye mwisho wa wakati, na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

227 Kama nilivyosema jana usiku, daima kuna matabaka matatu: wasioamini, wanaojifanya waaminio na waaminio. Na kulikuwako na Wasodoma, asiyeamini; kulikuwako na Lutu, anayejifanya mwaminio; na kulikuwa na Ibrahimu, lile Kanisa teule, lililoitwa litoke. Mnaona?

228 Sisi hawa hapa tumeketi leo, sisi hawa hapa leo, huyo hapo asiyeamini, Wasodoma, waangalieni huko nje, wanawake wakitembea mitaani wamevaa kaptura, wakivuta sigara, wakikata nywele zao, wanajiita Wakristo. Naam. Loo, jamani, wakifanya mambo haya yote, hata hivyo, wanajiita Wakristo, loo, naam, bwana, karamu, kucheza dansi. Wanaume wamepotoka, ninapata barua baada ya hapo...ushoga unaongezeka. Mnaona ninii...Ninapata takwimu zake za serikali, uliongezeka asilimia thelathini mwaka jana. Upotovu, mwenendo asilia wa maisha ya mwanadamu umepotoshwa, Sodoma. Waangalie watu baridi, wa kawaida moja kwa moja tu mle ndani, vile vile tu, wakigaagaa pamoja na nguruwe.

229 Mwangalie yule mjumbe aliyeshuka kwenda kule, wawili wao, Billy Graham wa kisasa, tuseme, akihubiri na kuwapofusha kwa Neno. Halafu kulikuwa na Kanisa ambalo halikufanya hivyo, lililoitwa litoke, lile Kanisa teule. Utukufu, utukufu! Lile Kanisa teule, Ibrahimu na kundi lake, Ni kitu gani kilichowatokea? Yule Mjumbe aliyemtokea Ibrahimu, akamwita vile jina lake lilivyokuwa ambalo Mungu alikuwa amempa siku chache tu hapo kabla, kutoka kwa Abramu likawa Ibrahimu, kutoka Sarai likawa Sara. Kisha kasema, "Yu wapi Sara, mkeo?" akamwita jina lake.

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

230 Kasema, "Nitakuzuru, Ibrahimu, kulingana na ahadi niliyokuahidi, muhula wake Sara." Ndipo Sara akacheka

kimoyomoyo, kidogo namna *hiyo*. Akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni Mungu.

231 Kama vile Yesu alivyosema, kabla ya wakati kufika ambapo lile Kanisa teule, lile Kundi la Kipentekoste . . . Sasa, Pentekoste si dhehebu. Sasa, ninyi ndugu mlio na Pentecostal Assemblies, Pentecostal Oneness, Pentecostal Church of God, Pentecostal Foursquare, na hayo yote, mnajipumbaza, hilo ni dhehebu, ambalo ni sawa, sina neno dhidi yake, bali ninyi sio hilo Kundi.

232 Pentekoste ni tukio ambalo Methodisti, Baptisti, Wapresbiteri, ambalo—ambalo Assemblies, na Foursquare, na Church of God, na ninii, mbona, Jina la Yesu, na hao wengine wote wanaweza kupokea, kama tu watalitii Neno la Mungu na kumfuata Yeye. Wataona mwujiza wa Mungu ambao utabadilisha maisha yao, na mambo hayo yatasambaratika nao watakuwa . . .

233 Mmethodisti anaweza kulipokea, Mkatoliki anaweza kulipokea, Mpresbiteri anaweza kulipokea. Ni Wakatoliki wangapi, ambao wakati mmoja walikuwa Wakatoliki? Inua mkono wako. Hivi Mkatoliki hawezi kulipokea? Ni Wabaptisti wangapi, pamoja nami? Wapresbiteri? Mnaona? Loo, la, hatuwezi kuliundia dhehebu. Anaenda kila mahali na kupata, "Yeyote atakaye na aje anywe katika Chemchemi ya . . . " Hiyo ni kweli. Loo, naam, bwana. Mnaona?

234 Sasa, Kanisa hilo teule, wote wameketi pamoja, mnaona, wote, bali Kanisa hilo teule litaiona ishara hiyo. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Ni wakati wa jioni. Mungu yuko wapi? "Kama Mungu yu pamoja nasi, iko wapi miujiza?" Sasa, Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Mnaamini hilo?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

235 Baba wa Mbinguni, kundi zuri sana la watu kuzungumzia, na huenda nisipate majaliwa haya tena, huenda nisiwe hapa tena, Ee Mungu, huenda tusione asubuhi ikija. Sayansi inajaribu kutwambia ya kwamba kuna nyota tano zitakazoanguka pamoja, hiyo ndiyo sababu wanasema, ulimwenguni kote, mataifa, wamegandia upande huu wa bara. Hii hapa Phoenix yenye mvua inayomwagika na hali ya hewa ambayo hawajawahi kuona. Wanadai ya kwamba nyota tano zinasogea pamoja huko nje. Wengine wanasema dunia itapasuka kama tikiti maji, hatuamini hilo, Bwana, kutakuwa na Utawala wa Miaka Elfu bado. Lakini wengine wanasema kutakuwa na matetemeko ya ardhi ambayo yatatikisa nyumba kila mahali, baadhi yao wanasema ya kwamba mawimbi makubwa ya bahari yatarushwa futi mia tatu hewani katika siku chache zijazo.

236 Ulimwengu unatetemeka. "Kutakuwako na matukio ya kutisha," Wewe ulisema, "katika siku za mwisho, matukio,

ishara mbinguni na duniani, moto, na mvuke, na nguzo za moshi, matetemeko ya nchi mahali mahali, mshangao wa wakati, dhiki kati ya mataifa, mioyo ya watu ikivunjika kwa hofu." Lakini wakati huo, Bwana, Wewe ulisema, "Inueni kichwa chenu, Ukombozi wenu unakaribia."

237 Sasa, Baba, tutainua kichwa chetu, usiku wa leo, juu ya madhehebu yetu, nitainua kichwa changu juu ya kundi ninaloshiriki, Wafanyabiashara Wakristo. Ninataka kila mtu, kila Mmethodisti ainue kichwa chake juu yake, kila Mbaptisti, kila Assembly, kila Foursquare, Umoja, ama Jina la Yesu, ama chochote walicho, Bwana, wainue kichwa chao juu yake. Angalieni huko ng'ambo ambako Yesu alisema, angalieni yale aliyosema "Kama mimi, nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu."

238 Ee Mungu, jalia tumwone ameketi huko ng'ambo, kwenye mkono wa kuume wa Ukuu wa Mungu, ameketi pale kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, usiku wa leo, akiishi daima, Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri, kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

239 Bwana, ndiyo kwanza nimalize kuhubiri, wakati nabii, ama mhubiri anapoenda na kulihubiri Neno, na kama halitimii basi msimsikie nabii huyo, hivyo ndivyo Neno Lako lisemavyo, lakini likifanya hivyo, likitimia, basi msikieni nabii huyo, "kwa kuwa niko pamoja naye."

240 Bwana, nimewaambia hao watu, usiku wa leo, ya kwamba Wewe ni Yesu yeye yule, jana, leo, na hata milele, Wakati wako umekaribia nazo Nuru za jioni zinaangaza, na mambo haya yote ambayo nimetangaza.

241 Sasa, Baba, lipe kundi hapa nje lililo na imani sasa ya kuliamini. Jalia ile imani iliyokuwa ndani ya Kristo, ile nia iliyokuwa ndani ya Kristo, ije ndani yetu. Na kama tuna nia ya Kristo, kama ninaweza kuwa na nia Yake ndani yangu usiku wa leo, kuna maskini mwanamke aliyeketi hapa ndani, labda, mahali fulani, ambaye anatokwa na damu, ambaye angeweza kumgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

242 Basi ikiwa nia Yake iko ndani yetu, Yeye atatenda vivyo hivyo, kwa sababu Yeye ndiye Kuhani Mkuu. Naye ni Neno la Mungu, Yeye ni Neno la Mungu, na kama Neno la Mungu linakaa ndani yetu, basi ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, kuhubiri mahubiri yatakayokata kabisa, ambayo yataweka shoka kwenye shina la mti, na Yeye pia ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.

243 Sasa, Baba, Neno Lako na lijulikane. Tunaliamini, kanisa hili dogo linaliamini, Bwana, watu hawa wanaliamini, mchungaji huyu analiamini, wachungaji hawa wengine wanaliamini. Tuko pamoja, usiku wa leo, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Wewe ulisema, "Walipo wawili watatu

wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa hapo katikati yao. Na kazi nizifanyazo, wao pia watazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bado, ninyi mtaniona," mwaminio, "kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi kote kote hata ukamilifu wa dahari." Ninakuamini Wewe, Bwana, Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

244 Sasa, Baba, kwa ajili ya kundi hili dogo nitafanyiza mstari wa maombi kuwaombea watu. Ninaomba ya kwamba Wewe utamponya kila mtu aliye katika jengo hili, usiku wa leo. Tujalie, Bwana. Jalia hawa manabii, walioketi hapa jukwaani, manabii huko nje mkutanoni, wanaume watauwa, wanaume walioitwa, wanaume waliotengwa, na mambo ya ulimwengu, wanawake waliotengwa, wasichana wadogo waliotengwa, wavulana wadogo waliotengwa, na roki hii yote na upuuzi wa ulimwengu, maskini wanawake na waungwana ambao kweli wamejazwa Roho, ambao ni wafuasi wa makanisa haya ya full Gospel, ambayo huacha nuru yao iangaze, wanawake ambao hawangevuta sigara wala kufanya jambo lolote baya bure, wakweli na waaminifu kwa Kristo na kwa mume wao, waume walio waaminifu kwa Kristo na mke wao na familia yao . . .

245 Bwana Mungu, Ibrahimu alisimama mwaminifu Kwako juu ya ahadi Yako, Uzao wa Ibrahimu, ambao ndio tulio kwa imani katika Kristo, tunasimama waaminifu kwa hiyo ahadi, Nawe ulijitambulisha kwa Ibrahimu kabla tu ya yule mwana aliyeahidiwa kutokea, yule mwana aliyeahidiwa alikuja baada ya ishara hiyo, sasa, Baba, tunamtazamia Mwana aliyeahidiwa, jalia hiyo ishara ionekane. Tujalie, Bwana. Mara tu Moto ukashuka, nasi tunautazamia wakati wowote, ishara ya mwisho, jalia iwe hivyo, Bwana, tunapojitolea sisi sote.

246 Ninalichukua kanisa hili dogo chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu, na katika Jina la Yesu Kristo, tunajiwasilisha Kwako, tupate kukuona Wewe hapa, Bwana, ushuhuda unaoonekana, ulio hai ya kwamba Yesu Kristo angali anaishi. Tujalie, Bwana.

247 Bariki kanisa hili dogo na maskini mchungaji wake mzuri, ninaomba, Mungu, Uwepo Wako utabaki hapa daima, na nguvu za Mungu zitaenea humu mjini kutoka mahali hapa. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

248 Ninasikitika kuwaweka kwa muda mrefu sana, hilo ni gumu sana na la kukatakata na kadhalika, na mtu yeyote anajua, anayenisikia nikihubiri, ya kwamba mimi si mhubiri. Mimi—mimi ni—mimi ni, sina elimu ya kuwa mhubiri, ama kujiita mwenyewe mhubiri, lakini, Ndugu, Dada, ninampenda Bwana Yesu, Yeye amenipa njia nyingine ya kuwajulisha ya kwamba ninawaambia ukweli. Kile kidogo nilicho nacho, ninajua habari Zake, sijui mengi kumhusu, ila ninajua kwamba ni halisi, mimi, ni halisi tu *kabisa*. Laiti ningejua yale watu fulani walijua kumhusu Yeye, labda hilo, ningeweza, Yeye angekuwa halisi

zaidi kwangu kama ningeweza kumjua Yeye kwa njia nyingine, lakini, kadiri ninavyomjua, ninajua Yeye hutimiza kila Neno ninalojua Yeye ameahidi, ninajua ni Kweli. Mungu awabariki.

249 Sasa hebu na tuimbe pambio moja dogo la wimbo, *Nampenda*. Ni wangapi wanaoujua wimbo huo wa kale? Kwa utamu tu kabisa sasa, kumwabudu katika Roho sasa:

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Sasa, wakati dada akiupiga huo kwa utamu. . .[Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

250 Weka tu nia yako Kwake sasa. Wanapoanza kuwaza juu Yake, Kleopa na rafiki yake walikuwa wakitembea siku moja wakinena habari Zake, ndipo akajitokeza moja kwa moja, akatembea pamoja nao siku nzima, hawakumjua Yeye, bali alipowafungia ndani, katika jengo dogo kama hili, alifanya jambo kama alilofanya kabla hajasulubiwa, hakuna mtu mwingine angaliweza kulifanya namna hiyo, ndipo wakajua ilikuwa ni Yeye. Lakini Yeye akatoweka machoni pao, akatoka mlangoni katika dakika moja tu. Mnaona? Walijua Bwana alikuwa amefufuka.

251 Jalia aje, usiku wa leo, na kufanya jambo fulani kama alilofanya kabla ya kifo Chake, ndipo tutajua, katika wakati huu, ya kwamba amefufuka katika wafu, kwa kuwa kama Yeye ni Yesu yeye yule, Yeye atatenda vile vile alivyotenda.

252 Sasa, tunapofanya jambo hili, tukivumisha, ninawatakeni, umshike mtu fulani mkono, anayeketi karibu nawe useme, "Dada, Ndugu, nitakuwa nikikuombea, upate kuponywa usiku wa leo, upate baraka zote za Mungu unazotaka." Semeni tu hivyo wakati ninyi, sisi kwa sisi tunapolifanya.

> Kwa sababu. . .

253 [Ndugu Branham anaondoka kwenye maikrofoni kuwasalimia wengine, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] (Mungu akubariki, Ndugu. . .?. . .Mungu akupe kila kitu unachotaka. . .?. . .)

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

254 Pamoja:

> Baba yetu, uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe.
> Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama huko Mbinguni.
> Utupe leo riziki yetu ya kila siku.

Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wanaotukosea.
Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu; kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

Na . . .

255 [Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham na kutoa ushuhuda—Mh.] Nenda, Da- . . . Naam, Mama. Naam, Mama. Amina. Mungu ashukuriwe. Asante.

256 Yeye yupo daima. Yeye si ni wa ajabu? Basi:

Nampenda, (Hivi Yeye si ni wa ajabu kumponya mama huyo?) Na . . .
Kwani . . . mimi
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Loo, Yeye ni wa ajabu, sivyo? Mungu asifiwe, wa ajabu *sana*. Vema.

257 Kadi za maombi, kutoka moja . . . Uligawa kadi za maombi moja hadi hamsini? Moja hadi hamsini, hebu tuchukue chache tu. Sasa, tunaninii tu . . . Tungeita wapi . . . ? Vema, ni kundi tofauti usiku wa leo, sivyo? Ni herufi zile zile? B na C. Hebu tuite kuanzia C, moja tupate kuona tunaweza kuwapata wangapi. Hebu tuite moja hadi kumi, moja B, au, C, moja. Moja, kadi ya maombi moja ni nani aliye nayo? Inua mkono wako. Huyo mama hapo anayo? Una kadi ya maombi . . . ? Tano. Vema, tano. Ni nani aliye na moja? Labda nilikosea. Nini? Vema. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Wasimamishe basi papa hapa.

258 Ninii tu, ninyi watoto wadogo mwaweza kurudi kwa namna fulani mlangoni, *pale*? Ama mje papa hapa, wapenzi, mkipenda, mkitaka kuja hapa jukwaani. Nadhani hilo lingekuwa sawa.

259 Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Hebu . . . Pangeni mstari kuanzia moja hadi kumi na tano, hebu tuanze nao, maana sisi, nina shaka kama mnaweza kuleta kiasi hicho humo ama hamwezi, kile tu mnachoweza kuleta. Huh? Mahali mnapopata . . . ? Moja hadi kumi na tano. (Sasa, Ndugu, kama mimi . . . imekuwa ni majaliwa kuwa hapa, usiku wa leo. Mungu akubariki, Ndugu.)

260 Vema. Ni wangapi humu jengoni sasa ambao hawana kadi ya maombi, na hata hivyo unataka Bwana Yesu akupe afya? Inueni mikono yenu. Kila mahali humu ndani ambao hawatakuwa kwenye mstari wa maombi, inueni mikono yenu mlio wagonjwa. Ni kote tu jengoni. Mngeweza . . . Sasa, angalieni, wakati wanapoingia, wa—watu wanapoingia mahali pao, ninawatakeni mfanye hivi, ninawatakeni mseme hivi sasa . . . Sasa kumbukeni,

kama—kama Hilo—kama Hilo si Neno la Mungu, basi silijui. Hiyo ni—hiyo ni ahadi.

261 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, sasa, hana budi kutenda kama vile alivyotenda, hana budi kuwa ndiye njia katika kila kanuni, ila tu mwili wa kawaida, maana mwili Wake wa kawaida ungali ni Dhabihu kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, Naye ameketi pale na mavazi Yake—Yake yaliyojaa damu ndiyo upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye, Mwenyewe, anatenda kama Kuhani Mkuu kufanya upatanisho juu ya yale tunayokiri kwamba Yeye amefanya. Mnaona?

262 Sasa, sio kwa kuhisi, ni kwa imani. Mnaona? Ungeweza tu kupigapiga, na kulia, na kadhalika, kamwe haitafanya kazi. Sio . . . Mimi . . . Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini?” Mnaona? “Uliamini?” Huna budi kuamini, kwa sababu, unaona, Yeye . . . huwezi kulifanya Neno lijipinge Lenyewe, halina budi kuendelea kikamilifu, kama tu vile bloku na kadhalika, mnaona, halina budi kuendelea kikamilifu, moja likishikana na lingine, unayaunganisha. Unaona? Huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo Kristo ni mkamilifu, kwa hiyo Neno Lake ni kamilifu. Sasa, Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri, tunakiri lolote alilotutendea, Yeye yuko kule mbele za Baba kulifanya sawa.

263 Angalia, kama Yona, katika tumbo la nyangumi, huku amefungwa mikono na miguu, magugu yote ya baharini yamemzunguka shingoni, matapiko ya nyangumi, labda kina cha pima arobaini ndani ya maji, kwenye bahari yenye dhoruba, akimtoroka Mungu, angeweza kugeuka kwenye tumbo la nyangumi huyo na kuangalia dalili zote alizokuwa nazo karibu naye, na kujua hali zake, na bado alisema zilikuwa ni ubatili wa uongo, “Mara nyingine tena nitatazama kukabili hekalu Lako takatifu,” naye Mungu akamdumisha hai siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi huyo . . . Mnaamini hilo kuwa ni kweli? Biblia kwanza inasema jambo hilo, naye Yesu alisema ilikuwa hivyo.

264 Sasa, angalieni, Yona . . . Yesu alisema mle katika Maandiko ya kwamba kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara. Hiyo ni kweli? Nao wangeona ishara, ishara ya Yona, “Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.” Ndipo Yona akatoka katika tumbo la nyangumi. Hiyo ni kweli?

265 Sasa, je, hiki ni kizazi kiovu na cha zinaa? Kimwili na kiroho pia? Uzinzi wa kiroho, uzinzi wa kimwili? “Kizazi kiovu, cha zinaa kitapokea ishara.” Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni ishara gani wakati huo? “Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, akafufuka, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika—katika tumbo la nchi, moyo wa nchi, kisha

afufuke." Basu ishara ambayo kizazi hiki kiovu na cha zinaa kingepata, ingekuwa ni ishara ya ufufuo. Hiyo ni kweli? Ishara ya ufufuo.

266 Sasa, ingekuwa nini basi? Ingekuwa ni Kristo aliyefufuka katika wafu, na baada ya miaka elfu mbili, angali hai, akitenda kazi pamoja na watu Wake, yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli?

267 Sasa, ni wangapi wa hawa wagonjwa . . .? Ni watu wangapi kwenye mstari wa maombi wanaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu? Inueni mikono yenu, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, mnaojua ya kwamba siwajui, wala kujua lolote kuwahusu. Ni wangapi kwenye hili kusanyiko wanaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu wala chochote kile? Mnaona? Simjui yeyote wenu, si kwenye mstari huu wa maombi, nitasema kwanza, huko nje.

268 Sasa, kuna watu fulani hapo ninaowafahamu. Ninamjua huyu, hawa, huyu, karibu kuanzia kwa yule—yule, kuanzia kwa maskini msichana yule mwenye nywele nyekundu pale, kuja huku, najua safu ile pale. Ndugu na Dada Dauch, hao wawili nyuma yao, ninawajua, wawili nyuma yao, ninawajua. Papa hapa, katika safu hii, papa hapa. Mmoja, wawili, watatu, wanne nyuma, ninawajua. Sasa, ninaamini, kama sijakosea, kama huyo si Ndugu na Dada Outlaw wanaoketi papa hapa nyuma, kutoka Kanisa la Jesus' Name, na Ndugu na Dada Sothmann, shemasi kutoka kanisa langu huko Jeffersonville, ama, mdhamini, hasa, kwenye halmashauri.

269 Sasa, si—sijui, ninaamini papa hapa kwenye kona hii, huyu kijana mwanamume na mwanamke, wanaoketi papa hapa, ninaamini huyo ni shemeji wa Ndugu Norman, ninasahau jina lake ni nani, hiyo ni kweli. Nje ya hao, sijui. Ndugu Williams na Ndugu Rose, na ndio kwanza tukutane na ndugu huyu hapa, na hiyo ni, nje ya hao, si—simjui mtu yeyote. Ninaamini wewe ni Dada Ungren, sivyo? Downing, Downing, hiyo ni kweli, kutoka Memphis. Vema. Mimi . . . Sasa, nje ya hao, na mwanangu, hata simwoni sasa, kwa hiyo, popote alipo, hao tu ndio niwajuao.

270 Sasa, mama wa kwanza mstarini ni yupi? Ni wewe moja kwa moja hapo? Loo, papa hapa? Wewe ndiwe mama wa kwanza. Vema. Waweza kusimama tu hapa kwa dakika moja?

271 Sasa, huyu hapa amesimama mwanamke ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Sasa, kama ningesema, "Huyu hapa ameketi mtu, ameketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, ameushika mkono wake, inaonekana kana kwamba umepooza ama chochote kile." Mnaona? Sijui ni kitu gani, umelemaa. Kama ningesema, "Mtu huyo ni kiwete," mtu yeyote anaweza kuona hilo. Mnaona? Lakini huyu hapa mwanamke anayeonekana mwenye afya na mwenye nguvu. Sasa, shida yake iko wapi? Hapo

ndipo mwujiza wako unapotokea, unaona, ndio huo, unaona, kitu fulani.

272 Sasa, kama—kama, vema, mimi, kama ningemwona mtu fulani amekunjamana kabisa, kifua chao kimezama ndani kabisa, akikohoa, sasa ningeweza kusema hiyo ilikuwa ni TB, huko kungekuwa ni kubahatisha. Mnaona? Basi mtu huyo huenda akasema, "Loo, la, sina TB." Mnaona? Na huenda ikathibitishwa ya kwamba hawana TB. Mnaona? Huwezi kujua. Lakini Mungu anaposema jambo lolote, ni kweli. Daima ni kweli, daima ni kweli.

273 Sasa, sasa, huenda mwanamke huyu anajifanya tu, huenda akawa tu anasema jambo fulani, huenda hata asiwe mgonjwa, huenda asiwe na tatizo lolote. Vema, si—sijui hilo, siwezi kusema. Ikiwa amesimama tu hapo, msijali, itagunduliwa katika dakika chache, mnaona, atajua, atagundua. Ni wangapi wamewahi kuwa mkutanoni na kuona hilo likifanywa? Loo, rehema, nimeona zaidi ya mia mbili ama mia tatu wakifa juu yake. Mnaona?

274 Namjua mtu, usiku wa leo, ameketi amepooza, amekuwa hivyo kwa miaka kadhaa. Nilipokuwa huko juu kwenye Jiji la Zion, wakati mtu huyo ameketi kule nyuma, akijaribu kunipumbaza akili mbele ya watu hao, niliendelea tu kujaribu kuendeleza mstari wa maombi, naye akaendelea kuketi pale, (Angeenda kwenye kambi za jeshi, mwajua, a—angewafanya hao wavulana, awapumbaze akili, awafanye wabweke kama mbwa, mwajua, na kutenda hayo.), niliendelea kuhisi roho hiyo ya ajabuajabu. Nao walikuwa—walikuwa wamemfanya aingie mle, kanisa linalojulikana.

275 Usiku kabla ya hapo, kulikuwa na m—mtu aliyekuja ambaye ni wa dhehebu *fulani*, akaja pale, naye alikuwa ameandika kwenye kadi yake ya maombi, "Nina TB, *hivi-na-hivi*," na yote namna hiyo, alidhani ilikuwa ni te—te—telepathia.

Kwa hiyo wao humkabidhi bawabu kadi ya maombi wanapokuja jukwaani, basi huyo mtu akaja pale nami nikasema, "Huna tatizo lolote."

Akasema, "Loo, naam, lipo, angalia kwenye kadi yangu ya maombi."

Nikasema, "Sijali kadi ya maombi inasema nini, huna tatizo lolote."

Akasema, "Vema, angalia, nina TB, na *ninii*," namna hiyo. "Angalia kadi hiyo ya maombi."

Nikasema, "Siangalii kadi hiyo ya maombi, ninaangalia kuelekea Mbinguni." Mnaona?

Naye akasema, "Vema, hiyo ndiyo shida yangu."

276 Nikasema, “Vema, labda, huenda ulikuwa nayo kule chini, kama unayo, hunayo sasa, kwa sababu wewe, haipo kabisa.” Naye akasema . . . Nikasema, “Huenda umeponywa huko chini.”

Akasema, “Uh-huh! Hivyo ndivyo unavyofikiria, ‘Umeponywa huko chini.’”

277 Nikawaza, “Mtu huyu ana shida gani?” Nikageuka na kuangalia tena, ndipo ono likatokea mbele zake, nikasema, “Ewe mdanganyifu! Wewe ni mfuasi wa kanisa *fulani*. Jana usiku uliketi na mtu pale *pale* juu aliye na suti nyekundu . . . aliye na tai nyekundu na suti nyeusi. Nawe . . . Huyo ni mke wake aliyeketi papa hapa kwenye kona *hii*, na mke wako. Nanyi mliketi karibu na meza iliyokuwa na kitambaa cha kijani kibichi, nanyi mkaamua kwamba mtakuja hapa kufanya hivyo kuthibitisha ya kwamba hii ilikuwa ni telepathia ya kiakili.” Nikasema, “Vitu ulivyoandika kwenye kadi yako viko juu yako.” Alikufa yapata majuma sita baadaye. Um-hum. Kamwe usifanye hivyo.

278 Mtu huyu, majuma machache baada ya hapo, siku chache usiku baada ya hapo, alikuwa ameketi pale akijaribu kunipumbaza, namna hiyo, nami nikaendelea kuhisi roho hiyo ya kigeni, nikasema, “Tafadhali, kila mtu, inamisha kichwa chako, iweni na kicho.” Mmenisikia nikisema hivyo mara nyingi, ninaangalia roho fulani, mnaona. Ndipo basi akaendelea kufanya hivyo, na kufanya hivyo, na moja kwa moja, akageuka namna *hiyo*, nikasema, “Kwa nini ibilisi ameweka moyoni mwako kufanya hivi?” Nikasema, “Uliingia ukitembea, lakini watakubeba ukitoka.” Nao wakafanya hivyo. Hiyo ni kweli kabisa.

279 Angali amepooza. Hiyo ni kweli. Alisimama tu, alikuwa amekakamaa, ilikuwa vigumu kwake kusogea. Naye ameandika barua baada ya barua, akiita, “Njoo.” Siwezi kufanya lolote kulihusu, hiyo ni dhambi yake mwenyewe, hana budi kusahihisha hilo na Mungu. Hakuna kitu, nisingeweka mkono wangu juu yake kwa chochote kile. Mnaona?

280 Vipi kuhusu yule mtu katika Phoenix, hapa chini, nilipokuwa hapa kwa mara ya kwanza wakati ule? Mnakumbuka huku, ambaye—ambaye asingeinamisha kichwa chake? Nao wakanivuta juu yake mara dazani moja huko California, akiketi mle, amejaa mandevu, afisa hapa mjini, ndevu zimejaa usoni mwake, namna hiyo, ameketi pale akifanya, “Uhhh, uhhh,” namna hiyo, hana akili hata kidogo, pepo mchafu alitolewa katika mtu mmoja na kuingia ndani yake. Hiyo ni kweli. Papa hapa Phoenix, safari yangu ya kwanza. Hiyo ni kweli. Mnaona, inakubidi tu kuwa mwangalifu, sasa, hatuigizi kanisa.

281 Ni kama tu ilivyokuwa katika siku za Gideoni, wakati wa kuigiza kanisa umekwisha, hatuna budi kujiandaa kukutana na Mungu. Naam, bwana. Kuzunguka-zunguka, kuandika jina lako kwenye tiketi, na kujiunga na kanisa, hayo yote ni bure.

Kumbukeni vitu hivi vitatoka kwa mmoja vimwingie mwingine, bila shaka vitatoka.

282 Huyu mwanamke simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Yeye, kama ni mgonjwa, sijui lolote kulihusu. Je, anataka maombi kwa ajili ya mtu mwingine? Sijui chochote juu yake, ni juu tu, ni juu ya Mungu kusema hivyo. Lakini kama Yeye atasema hivyo, na awe mwamuzi kama ni kweli ama si kweli.

283 Je, utaamini, basi, ya kwamba Kuja kwa Kristo kumekaribia, na Roho Mtakatifu yeye yule, Mungu yeye yule, aliyekuwa huko chini Sodoma, ni Mungu yeye yule Ambaye anatokea hapa nyuma katika wanaume na wanawake, usiku wa leo? Unaamini hilo, mambo aliyosema Yeye? Amini, amini.

284 Sasa, ninamtaka aangalie jinsi anavyoangalia, ili msione, msifikirie nilikuwa nikisoma-. . .Mtu yeyote. . .Watu husema ninasoma mawazo ya watu. Loo, kwa. . .Mtu yeyote ambaye angalau anajua jambo la kwanza la hayo, anajua ya kwamba hiyo kabisa ni. . .Mbona, telepathia ni, unakisia namba na hebu niikisie pia. Mnaona? Hakuna—hakuna kitu kama hicho. Jamani! Mungu si telepathia.

285 Walimwita Yesu Beelzebuli kwa sababu alifanya hivyo, walisema alikuwa ni mpiga ramli, ibilisi. Akasema, "Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, ulimwengu huu, wala Ulimwengu ujao." Kwa hiyo mnaona mahali linapotuweka? Unaelewa hilo, sivyo, Dada? Sisi sote tunaelewa.

286 Sasa, sisemi ya kwamba atafanya hivyo, ninatumaini ya kwamba atafanya, maana sikujui, wala wewe hunijui, na sisi hawa hapa tumesimama, usiku wa leo. Na kama ningalikuwa na nguvu kuninii, kama wewe ni mgonjwa nami nilikuwa na nguvu za kukuponya, ningefanya hivyo. Kama ningekwambia, ningesema uongo. Jambo pekee ninaloweza kufanya ni kuwaambia ya kwamba Neno linasema ya kwamba kwa kupigwa Kwake mliponywa. Hiyo ni kweli, mliponywa.

287 Ninaweza kuwaambia sasa, huyu mwanamke si mwenye dhambi, yeye ni Mkristo. Naam, ana mtetemo mzuri rohoni mwake. Mnaona? Yeye—yeye ni Mkristo, naye anaugua yabisi kavu. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, "Naam. Tangu kufanyiwa upasuaji."—Mh.] Naam, bwana. Na upasuaji huo ulikuwa ni upasuaji wa kibofu nyongo, basi ulipokuwa na huo, uliogopa kidogo kwamba—kwamba upasuaji huo ulikuwa na uhusiano fulani na huu, nawe umefadhaika sana tangu wakati huo. Una magonjwa mengi ya ziada. Hiyo ni kweli. Sasa, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya? Toka tu mumu humu jukwaani na kusema, "Asante, Bwana," na uendelee. Amina.

288 U hali gani, Mama? Hatufahamiani, Mungu anatujua sote wawili. Lakini kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Si kwa ajili yako, ni kwa ajili ya mtu mwingine, mpwa wako. Nenda ukaamini.

Unaamini kwa moyo wako wote? Amini, usiwe na shaka.

289 Njoo, Mama. Sasa, imeanza katika kusanyiko. Sasa, imani yako imeanza kupanda, unaona, unaweza kuihisi, wewe, ninii tu—Kitu fulani tu kinaanza kuvuta, unaona. Kila kitu, ninaangalia huko nje na inaonekana tu kama hiki chumba kimeanza kugeuka kama taa ya kaharabu, mwajua, nikiangalia tu pande zote.

290 Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, hilo lisingekuathiri namna hiyo." Kama maskini mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi la Yesu na kumdhoofisha Mwana wa Mungu, ingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Mnaona? Iweni tu na imani.

291 Hatufahamiani. Sikujui, lakini kama Bwana Yesu atanifunulia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Nawe unaamini ya kwamba yale niliyosema, ni thibitisho la yale Mungu aliyoahidi? Unaamini? Vema. Tatizo lako liko ubavuni mwako. Hiyo ni kweli. Umefanyiwa upasuaji, kansa. Umedhoofika sana. Hiyo ni kweli. Unashangaa kuna nini. Lakini utakuwa mzima sasa. Vema, Mungu. . .?. . . sasa, kama anaweza kukwambia kile ambacho kimekuwa. . . Hiyo ilikuwa ni kweli? Vema, kama anaweza kukwambia kile kilichokuwako ni kweli, basi anachosema katika siku za usoni ni kweli. Unaona?

U hali gani? U hali gani? Hatufahamiani, sikujui. Ni kwa ajili ya mvulana huyo? Vema. Hebu kidogo.

292 Sasa, kuwa tu na kicho kabisa na uamini kwa moyo wako wote ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye atatimiza yaliyosalia, kama tu unaweza kumwamini Yeye.

293 Ulipangusa macho yako basi, Dada, ukiomba. Lakini huo ugonjwa wa matumbo umekuacha. Amini tu sasa, kwa moyo wako wote. Amini. Tayari unajisikia tofauti, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili watu waweze kuona.

294 Ninataka kuwaulizeni, huyo mwanamke alimgusa Nani? Hakunigusa kamwe, yeye yuko mbali sana, mnaona. Lakini alimgusa Kuhani Mkuu, hiyo ni kweli, alimgusa Kuhani Mkuu.

295 Una wasiwasi kuhusu huyo mvulana, kitu kama figo, kibofu. Je, mume wako ameshamwombea? Anapaswa, kwa kuwa ni mhudumu. Atakuwa mzima, usiwe na wasiwasi.

Yesu si ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

296 Je, unaona ile Nuru inayoning'inia juu ya mtu huyo anayeomba? Hayo maumivu ya kichwa, yatakuacha, nawe

utakuwa mzima sasa. Usiwe tu na shaka, amini, yote yataondoka. Ulikuwa ukiomba Yeye afanye hivyo, sivyo? Hiyo ni kweli, ukisema, "Bwana Yesu, mwombe Ndugu Branham aniite." Vema. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Vema, yote yamekwisha.

Hilo lilimfanya huyo mtu nyuma yako, aamini. Tatizo hilo miguuni mwako litaondoka pia, ndugu, kama wewe . . .

297 Anaweza kuponya pumu pia, sivyo? Aiponye. Vema. Nenda tu ukamwamini kwa moyo wako wote. Iweni . . . Usiwe na shaka, amini tu kwa moyo wako wote. Vema.

Mnaamini huko nje sasa? Msiwe na shaka. Kuna roho wa kipekee anayeingia humu ndani, ninatumaini ya kwamba Bwana Yesu atalirekebisha. Vema.

Vema. Endelea, ukiamini sasa, Dada.

Vema, Mvulana Mdogo. Ni kwa ajili yake? Ni . . . Naam. Wasemaje? Naam, endelea moja kwa moja nayo itamwacha, hiyo pumu, naye atakuwa mzima na apate afya.

Vema. Unaamini, Dada? Shida ya wanawake itakuwa sawa. Nenda, na uamini kwa moyo wako wote.

Amini sasa.

Njoo, Dada. Unaamini Mungu huponya ugonjwa wa moyo? Anaweza kuponya wako pia, sivyo? Kwa hiyo nenda tu ukiamini . . . ? . . .

298 U hali gani, Bwana? Unataka kwenda kula chakula chako cha jioni? Endelea ukale. Mungu akubariki. Yote yamekwisha, wasiwasi, ugonjwa wa tumbo umekwisha, yote yamekwisha. Kuwa tu na imani, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

299 Wewe ni mtu mkubwa sana anayeonekana mnene, kuugua wasiwasi, lakini hivyo ndivyo ilivyo. Utakuacha sasa. Nenda ukaamini kwa moyo wako wote.

300 Mtu huyo aliyeketi huko nyuma na kivuli hicho cheusi, na mvulana huyo mdogo aliyeketi moja kwa moja huko nyuma aliye na kifafa, unaamini, Mwanangu, kwamba Mungu atakuponya? Unataka kuliamini? Vema, mwamini Mungu nacho kitakuacha.

Haleluya! Unaamini? Amina.

301 Kumwombea mvulana mdogo, la, ni kuomba, mwanamke huyo wa Kimeksiko, akimwombea mwana aliye na kansa, ambaye hajaokoka. Kama utaamini, Mungu atalishughulikia. Mwaminini Mungu, msiwe na shaka. Um-hum.

302 Uvimbe, hivi unaamini ya kwamba Mungu atashughulikia huo uvimbe, unayeketi moja kwa moja mbele ya huyo mwanamke hapo aliyekuwa na uvimbe, ninyi wawili mlioketi pamoja, amini kwa maisha yako yote, kwa moyo wako wote, nawe unaweza kupata kile ulicho nacho. Amini kwa moyo wako wote.

303 Huyo mvulana hapo aliye na kifafa, unaamini ya kwamba Mungu atashughulikia hilo? Maskini jamaa huyo aliyeketi upande wa ndani, mvulana huyo aliyeketi hapo, mwekee mkono, Bwana. Amini kwa moyo wako wote.

Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake, Shetani! Huwezi kujificha.

304 Shetani hawezi kuficha chochote sasa, Uwepo wa Bwana upo hapa. Unaamini kwa moyo wako wote? Je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Ni kitu gani? Amini, tenda kulingana na Neno Lake ukitaka kuona miuji-. . . "Kama Mungu yu pamoja nasi iko wapi miujiza Yake?" Hii hapa! Mungu yu pamoja nasi. Amina. Mungu yu pamoja nasi. Hii hapa ishara ya kwamba Yeye yu hai, jambo lile lile alilofanya kabla hajafa. Amefufuka milele.

305 Sasa, mnaninii. . .? Je, ninyi ni waaminio? Inua mkono wako. Loo, jamani! Wekeaneni mikono. Usijiombee mwenyewe, mwombee mtu mwingine. Anza tu kuomba, omba tu, "Bwana Mungu, mponye mtu huyu, huyu mtu mwingine." Jambo ndilo hilo, aminini sasa.

306 Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tunaomba kwamba nguvu za Mungu zipitie kwenye jengo hili sasa, kama upepo wa nguvu ukienda kasi na kuijaza nyumba hii yote, na kuwajaza watu hawa na Roho Mtakatifu wa nguvu kuamini ya kwamba Mungu angali anaishi na kutawala.

Shetani, toka mahali hapa, toka kwa watu hawa, ninakuapisha, katika Jina la Mungu Aliye Hai. Amina.

307 Hebu na ishikilie, hebu izame ndani. Mwaminini Yeye. Anawezaje kushindwa? Hawezi kushindwa. Kama anaweza kusimama hapa jukwaani na kufanya hivyo, ni zaidi sana vipi anavyoweza kuwafanyia?

308 "Ndugu Branham, unafanyaje hivyo?" Hilo ni Neno Lake. Hilo ni Neno Lenyewe likidhihirishwa. Neno litajidhihirisha Lenyewe ndani yako, kama utaliamini. Ondoa mawingu ya mashaka, Mwana anaangaza, M-w-a-n-a anaangaza, nguvu Zake ziko humu chumbani kumponya kila mmoja wenu. Amina.

309 Unaamini hilo? Moyo wako wote? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, simama na ulikubali, katika Jina la Yesu Kristo. Inueni mikono yenu na kumsifu, mpeni sifa.

Vema, Mchungaji. . .?. . .

62-0124 Siye Mimi Niliyekutuma?
Assembly Of God
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org